
Nipashe
Jumatatu Oktoba 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581479
MWANGA WA JAMII
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com



UKURASA 22 **KANE ALIFURAHISHWA NA BAO LA AJABU**

UTAFITI WABAINI...

# 15% ya walioolewa wana wake wenza



• **Asilimia** sita ya waume nchini wana wake zaidi ya mmoja; Dar hatari kwa ujauzito kuharibika... *Endelea ukurasa 2*



> **Miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 20-49, asilimia saba wana uzito pungufu na asilimia 36 wana uzito uliozidi au uliokithiri.**

UKURASA WA 3

**EU YAIPA TANZANIA BIL. 95/- UTEKELEZAJI MRADI UMEME**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 36...

## Kipimo kubaini hatua ya awali saratani matiti chaletwa Z'bar

UKURASA 17

UKURASA WA 7

**Matinyi:** Hakukuwa na usiri utiaji saini uwekezaji Bandari

UKURASA WA 4

Hatifungani ya Kijani ya CRDB yakusanya Bil.170/-, yaorodheshwa DSE



UKURASA WA 19

**Iran** yaionya Israel uvamizi Palestina



## TMA yatoa tahadhari ya mvua kubwa kuanzia leo

UKURASA 3

**MICHEZO** BALEKE, AZIZ KI RAHA DABI SIMBA, YANGA UK.24

**KATUNI** UK.6

**HABARI KITAIFA**



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Kipunguni wakiwa katika vikundi vya kuibua mbinu zinazotumika mitaani kuendeleza ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike, katika kikao maalum kilichoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Utafiti: Asilimia 15 ya walioolewa wana mke mwenza mmoja au zaidi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAKWIMU za Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa mwaka 2022 (DHS-MIS 2022) zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara za Afya, zinaonesha asilimia 15 ya wanawake walioolewa wana mke mwenza mmoja au zaidi huku asilimia sita ya wanaume wana wake wawili au zaidi.

Ripoti hiyo iliyozinduliwa mwishoni mwa wiki na Rais Samia Suluhu Hassan, ilihusisha wanawake 15,254 wenye umri kati ya miaka 15-49 kutoka kwenye kaya 15,705 zilizochaguliwa na wanaume 5,763 waliofanyiwa mahojiano wenye umri kati ya miaka 15-49 kutoka katika nusu ya kaya zilizochaguliwa.

Utafiti huo unaonesha kuwa ndoa za mitaala zipo zaidi kwa wanawake na wanaume ambao hawana elimu na wanaoishi katika kaya maskini.

**HALI YA UKATILI**

Ripoti hiyo pia inaonesha asilimia 27 ya wanawake wa Tanzania wenye umri wa miaka 15-49 wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili tangu wakiwa na umri wa miaka 15.

Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kabla ya utafiti, asilimia 18 ya wanawake walifanyiwa ukatili wa kimwili na zaidi ya theluthi moja (asilimia 35) walioolewa au wanaoishi na wenza wa karibu, wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili, ikilinganishwa na asilimia nne ya ambao hawajawahi kuolewa.

Miongoni mwa wanawake walioachika, kutengana, au wajane, asilimia 50 wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili huku waliowahi kuolewa au kuwa na mpenzi/mwenza/mtu wa karibu, watuhumiwa wa ukatili wa kimwili ni wanaume wa sasa na wa zamani/wapenzi. Mama/mama wa kambo na baba/baba wa kambo ndio watuhumiwa wa ukatili wa kimwili miongoni mwa wanawake ambao hawajawahi kuolewa wala kuwa na wapenzi.

Asilimia 12 ya wanawake nchini wenye umri wa miaka 15-49 wamewahi kufanyiwa ukatili wa kingono ikijumuisha asilimia saba ya wanawake waliofanyiwa ukatili huo katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti. Asilimia 22 ya wanawake walioachika, kutengana, au wajane wamewahi kufanyiwa ukatili wa kingono.

Takribani nusu ya wanawake (asilimia 49) waliofanyiwa ukatili wa kimwili au wa kingono hawakuwahi kutafuta msaada na hawakuwahi kumwambia mtu yeyote. Vyanzo vikuu vya msaada ambavyo wanawake walivitumia ni familia zao (asilimia 62) na familia ya wanaume au wapenzi wao (asilimia 39).

Kuhusu ukatili baina ya wenza, utafiti unaonesha wanawake wawili kati ya watano waliowahi kuwa na wenza wamepitia ukatili wa kimwili, kingono, au kihisia kutoka kwa mume au mwenza wa sasa au hivi karibuni.

Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kabla ya utafiti, asilimia 33 ya wanawake ambao wamewahi kuwa na wenza walifanyiwa ukatili na mume/mpenzi. Hii inajumuisha asilimia 22 waliopata ukatili wa kihisia, asilimia 24 ya ukatili wa kimwili, na asilimia tisa walipata ukatili wa kingono.

Ukatili uliofanywa na mume au mwenza wa hivi karibuni ni mkubwa zaidi katika maeneo ya vijijini (asilimia 34). Vitendo vya ukatili ni zaidi ya mara mbili kwa Tanzania Bara (asilimia 33) kuliko Zanzibar (asilimia 15). Kimkoa, ukatili wa hivi karibuni wa wenza ni kati ya asilimia tisa ya wanawake wa Kaskazini Unguja na Kusini Pemba hadi asilimia 64 kwa wanawake wa Mkoa wa Mara.

# ...Dar hatari ujauzito kuharibika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MATOKEO ya ujauzito na utoaji wa mimba katika Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa mwaka 2022, yanaonesha asilimia 23 ya mimba Mkoa wa Dar es Salaam ziliharibika.

Kiwango hicho kimeeleza ni kikubwa kuliko mkoa wowote huku cha chini zaidi (asilimia moja) kilikuwa Mkoa wa Rukwa.

Ripoti ya utafiti huo iliyozinduliwa juzi na Rais Samia Suluhu Hassan, ilihusisha wanawake 15,254 wenye umri kati ya miaka 15-49 kutoka kwenye kaya 15,705 zilizochaguliwa na wanaume 5,763 wenye umri kati ya miaka 15-49 kutoka katika nusu ya kaya zilizochaguliwa walifanyiwa mahojiano na imetolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara za Afya.

Matokeo hayo yanaonesha kuwa taarifa za ujauzito kwa wanawake wenye umri wa kati ya miaka 15-49 kwa kipindi cha miaka mitatu kabla ya utafiti huo asilimia 90 walizaa watoto hai na asilimia 10 walipoteza ujauzito.

Kati ya wanawake waliopoteza ujauzito asilimia nane mimba zao ziliharibika, asilimia mbili walizaa watoto wafu na asilimia chini ya moja walitoa mimba huku asilimia 23 ya mimba katika Mkoa wa Dar es Salaam ziliharibika, kikiwa ni kiwango kikubwa kuliko mkoa wowote na cha chini zaidi (asilimia moja) kilikuwa mkoa wa Rukwa.

**NJOMBE KINARA UZAZI WA MPANGO**

Ripoti hiyo inaonesha wanawake wengi walioolewa Tanzania Bara wanatumia njia za kisasa za uzazi wa mpango ikilinganishwa na wa Zanzibar (asilimia 32 kwa asilimia 17 mtawalia) huku wanawake wengi walioolewa wanaoishi mjini hutumia njia za kisasa zaidi (asilimia 35) ikilinganishwa na vijijini (asilimia 29).

Mikoa ya Simiyu na Kaskazini Unguja ina asilimia ndogo ya wanawake walioolewa wanaotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango (asilimia tisa kwa kila mkoa) huku matumizi yakiwa makubwa kwa Mkoa wa Njombe (asilimia 56).

**UZITO ULIOZIDI WANAWAKE**

Utafiti wa mwaka 2022 ulikusanya vipimo vya uzito na urefu kutoka kwa wanawake wenye umri wa miaka 15- 49 na miongoni vijana balehe wanawake, asilimia 18 wenye umri wa miaka 15-19 wana ukondefu na asilimia 12 wana uzito uliozidi au uliokithiri.

Miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 20-49, asilimia saba wana uzito pungufu na asilimia 36 wana uzito uliozidi au uliokithiri. Hali ya uzito uliozidi au uliokithiri miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 20-49 inaonekana kuongezeka kadiri elimu na hali ya uchumi wa kaya inavyoongezeka.

Utafiti huo ulikusanya taarifa za ulaji wa vyakula na vinywaji miongoni mwa wanawake siku moja kabla ya utafiti, asilimia 25 ya wanawake wamekula kutoka makundi matano ya vyakula miongoni mwa makundi 10 yaliyoainishwa na kukidhi mahitaji ya mchanganyiko wa vyakula unaokidhi kiwango cha chini kinachokubalika kwa wanawake.

Aidha, zaidi ya robo (asilimia 28) ya wanawake walitumia vinywaji vilivyoongezwa sukari na asilimia 14 walikula vyakula visivyo salama kiafya siku moja kabla ya utafiti.

**HALI YA UZAZI**

Ripoti hiyo pia imeonesha kuwa wanawake nchini wanazaa wastani wa watoto 4.8. Hata hivyo, takwimu za kimkoa zinaonesha uzazi unatofautiana kutoka wastani wa watoto 2.8 kwa mwanamke katika Mkoa wa Dar es Salaam hadi wastani wa watoto 6.6 kwa Mkoa wa Simiyu.

Utafiti ulihusisha wanawake 15,254 wenye umri wa miaka 15-49 kutoka kwenye kaya 15,705 zilizochaguliwa na wanaume 5,763 wenye umri wa miaka 15-49 kutoka katika nusu ya kaya zilizochaguliwa walifanyiwa mahojiano.

Kwa ujumla, kiwango cha uzazi kimepungua kutoka wastani wa watoto 6.2 mwaka 1991-92 hadi watoto 4.8 kwa mwanamke mwaka 2022.

Wanawake wanaoishi katika maeneo ya vijijini wana uwezo wa kuwa na watoto wengi kuliko wanawake wa maeneo ya mijini (wastani wa watoto 5.5 dhidi ya 3.6 mtawalia).

Kiwango cha uzazi nchini kinapungua kulingana na ongezeko la kiwango cha elimu kutoka wastani wa watoto 6.3 kwa wanawake ambao hawana elimu hadi wastani wa watoto 3.8 kwa wanawake wenye elimu ya sekondari na zaidi.

Kadhalika, utafiti huo umeonesha kuwa kiwango cha uzazi kinapungua kadri hali ya uchumi wa kaya unavyoongezeka.

Wanawake wanaoishi kwenye kaya za uchumi wa chini wana wastani wa watoto 6.7 kulinganishwa na wanawake kutoka kwenye kaya zenye uchumi wa juu (wastani wa watoto 3.3).

Pia, inaonesha nusu ya wanawake wenye umri wa miaka 25-49 wameolewa kwa mara ya kwanza wakiwa na wastani wa umri wa miaka 19.8 huku wanawake wa vijijini wanaolewa mapema zaidi (miaka 19.2) kulinganishwa na wanawake wa mjini (miaka 21.4).

Wanaume wanaoa miaka tano baadaye zaidi ya wanawake. Wastani wa umri wa kuoa kwa wanaume wenye umri wa miaka 25-49 ni miaka 24.9. Wastani wa umri wa kuanza kujamiiana kwa mara ya kwanza ni miaka 17.0 kwa wanawake wenye umri wa miaka 25-49, na wastani wa miaka 18.6 kwa wanaume wenye umri huohuo.

Theluthi mbili ya wanawake na asilimia 41 ya wanaume wenye umri wa miaka 25-49 walijamiiana kabla ya umri wa miaka 18, na asilimia 14 ya wanawake na asilimia saba ya wanaume wenye umri wa miaka 25-49 walijamiiana kabla ya miaka 15.

Wanawake wanaoishi vijijini walianza kushiriki tendo mapema kwa wastani wa mwaka mmoja (miaka 0.9) kulinganishwa na wanawake wa mijini.

Wastani wa umri wa kuzaa kwa wanawake wenye umri wa miaka 25-49 ni miaka 19.9. Hii ina maana kuwa nusu ya wanawake wenye umri wa miaka 25-49 hupata watoto wa kwanza kabla ya kufikia umri huo.

Kwa wastani, wanawake wa mjini hujifungua kwa mara ya kwanza miaka 1.2 baadaye kulinganishwa na wanawake wa vijijini (miaka 20.8 kulinganisha na 19.6).

# TMA yatoa hadhari mvua kubwa leo

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa tahadhari kwa wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mafia, Unguja na Pemba kuhusu uwezekano wa kunyesha mvua kubwa katika baadhi ya maeneo yao kuanzia leo hadi keshokutwa.

Katika taarifa yake ya jana, mamlaka hiyo ilisema mvua hiyo inaweza kusababisha mafuriko na kuharibu shughuli za kiuchumi za wananchi, hivyo kuwaelekeza wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kuchukua tahadhari na kujiandaa kwa dharura inayoweza kujitokeza.

Julai 29 mwaka huu, TMA ilitabiri uwezekano wa kuwa na mvua ya El-Nino katika katika kipindi cha msimu wa vuli. Inatarajiwa kuanza mwezi Oktoba hadi Desemba mwaka huu.

Mamlaka hiyo ilitoa angalizo kuwa mvua hiyo inaweza kusababisha athari katika maeneo mbalimbali nchini.

Ilibainisha kuwa mvua hiyo inaweza kuleta madhara kwa binadamu na mazingira ikiwamo vifo, mafuriko, ardhi kuporomoka, upotevu wa mali, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu hivyo kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Agosti 31 mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema serikali imezielekeza kamati za usimamizi wa maafa na sekta, kushirikiana na umma kuchukua hatua kukabiliana na madhara yanayoweza kutokea.

Alitaja hatua hizo kuwa ni kutambua maeneo hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuandaa mipango ya kuzuia madhara na kukabiliana na maafa endapo yatatokea pamoja na kuainisha na kuandaa rasilimali za usimamizi wa maafa kwa kila sekta kushiriki kikamilifu katika eneo lake.

"Tunazielekeza kamati hizo zisisubiri maafa yatokee, waanze kutambua maeneo yote hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuanza kuandaa mipango ya kuzuia madhara yoyote yanayoweza kutoka na utabiri huo wa TMA," aliagiza.

Vilevile, Oktoba 13 mwaka huu, Ofisi ya Waziri Mkuu ilizindua Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kuzuia na Kukabiliana na Madhara ya El-Nino na kuusambaza kwa viongozi wakuu wa serikali wakiwamo mawaziri, makatibu wakuu na taasisi za serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake.

# EU yaipa Tanzania bil. 95/- utekelezaji mradi umeme

**Na Jenifer Gilla**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 36 (Sh.bilioni 95) kwa ajili ya utekelezaji Mradi wa Uzalishaji wa Umeme kwa njia ya maji wa Kakono, mkoani Kagera wa megawati 87.8.

Utiaji saini wa mkataba huo kati ya EU na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), ulifanyika katika Mkutano wa Global Gateway Forum, Brussels nchini Ubelgiji na kushuhudiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo.

Akizungumza baada ya utiaji saini huo uliofanyika Oktoba 25 na 26, mwaka huu, Prof. Mkumbo aliishukuru EU kwa kuipatia Tanzania msaada huo na kuahidi serikali itausimamia utekelezaji wake ipasavyo.

Alisema kwa ujumla mradi huo umegharimu Euro milioni 288.11 sawa na Sh. bilioni 800 zilizotokana na mikopo nafuu kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na msaada wa EU.

Prof. Mkumbo pia alishiriki mijadala ya kuweka mikakati ya pamoja kwenye madini ya kimkakati na mageuzi ya kidijitali na kukubaliana kwamba Mpango wa Global Gateway uchochee uwekezaji wa kuongezewa thamani ya madini nchini yanakochimbwa badala ya kuongezwa nje yanakokwenda kuuzwa.

Waziri aliishukuru EU kwa msaada wa Euro milioni 35 (Sh. bilioni 80) ilizotenga kuisaidia Tanzania kwa ajili ya kuchochea mageuzi ya kidijitali na msaada Euro milioni 703 (Sh. trilioni 1.9) ilizopanga kusaidia kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo nchini kwa mwaka 2021 hadi 2027.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BEATUS MANOTA IDAMA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 845 CUU – TOYOTA VEROSA yenye Chassis No. GX1106033650. Engine No. IG6097290. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi: PHQ/ARU/ARU/5061/2023.

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**IRINGA QUALITY PRODUCTS LIMITED** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI MBILI ZA GARI ZENYE USAJILI T954CGS MERCEDES BENZ-815 ATEGO, T844BZX IVECO-STRALIS.YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE.

POLISI JALADA **PHQ/IRI/IRI/2570/2023, PHQ/IRI/IRI/2569/2023.**

## MNADA WA HADHARA:

**TAREHE 10/11/2023** Kwa idhini tuliyopewa na mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya **MUFINDI-MAFINGA** kufuatilia shauri la madai No 5/2023 la **MPEPWA MICRO FINANCE- MDAI** dhidi ya **ZHANG MIN- MDAIWA.** Tumeamriwa kuuza kwa mnada wa hadhara mali ya mdaiwa kama ifuatavyo: Gari No **T 518DPL TOYOTA PRADO-TX** Gari lipo kwenye hali nzuri Mnada utafanyika siku ya Ijumaa Tarehe 10/11/2023 eneo la Yard ya Majembe Kihesa Masharti ya mnada:

(a) Ukaguzi wa gari unaruhusiwa siku mbili kabla ya mnada

(b) Mnunuzi atalazimika kulipa si chini ya 25% ya bei aliyofikia kwenye mnada na salio lilibakia lilipwe ndani ya siku kumi na nne(14)

(c) Ikiwa Mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda aliopewa atakuwa amepoteza haki zake zote na gari litauzwa upya.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na ofisi yetu iliyopo Yard ya Majembe Auction Mart Ltd Kihesa Simu +255 764 464 746 au + 255 764 430 413**


## Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

#### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-23 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-23 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,859 | 1,519 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 10,830 | 15,483 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 57,018 | 49,545 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,021 | 4,010 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 8,924 | 13,559 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 102,981 | 101,464 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,883 | 2,708 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,062 | 2,227 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **192,578** | **190,515** |
| B. | B. **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 44,234 | 54,395 |
| 18 | Amana za Wateja | 104,176 | 92,438 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 15 | (108) |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,104 | 3,197 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,370 | 1,449 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **152,925** | **151,396** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **39,653** | **39,119** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,786 | 1,420 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 14,108 | 15,473 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,260 | 726 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **39,653** | **39,119** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 25,260 | 15,496 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 7,870 | 7,600 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,159 | 678 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20.59% | 20.53% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.56% | 7.44% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 70.17% | 69.56% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 53.47% | 53.26% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.32% | 86.74% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.07% | 3.88% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1.08% | 3.00% |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 30-Sep-23 | 30-Sep-22 | 30-Sep-23 | 30-Sep-22 |
| 1 Mapato ya Riba | 4,175 | 3,168 | 11,856 | 9,635 |
| 2 Gharama za Riba | 1,978 | 1,391 | 5,797 | 3,822 |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba ( 1kutoa 2)** | **2,197** | **1,777** | **6,059** | **5,813** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (6) | (31) | (841) | (36) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 481 | 351 | 1,899 | 932 |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **423** | **221** | **1,020** | **592** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 91 | 51 | 234 | 139 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 332 | 170 | 786 | 453 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,476** | **1,438** | **4,357** | **4,153** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 763 | 691 | 2,169 | 1,925 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 713 | 747 | 2,188 | 2,228 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **669** | **240** | **1,664** | **1,356** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 135 | 187 | 404 | 560 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **534** | **53** | **1,260** | **796** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka** | **534** | **53** | **1,260** | **796** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 34 | 34 | 34 | 34 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 99 | 10 | 78 | 74 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.39% | 0.58% | 1.19% | 1.60% |
| (ii) Wanahisa | 5.42% | 0.56% | 4.33% | 4.20% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 32.10% | 42.43% | 33.84% | 40.61% |
| (iv) Zinazozalisha | 5.26% | 5.11% | 5.00% | 8.01% |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.07.2023** | **21,500** | **-** | **16,199** | **1,420** | **-** | **-** | **39,119** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 534 | - | - | - | **534** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,366) | 1,366 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | - | | | | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.09.2023** | **21,500** | **-** | **15,366** | **2,786** | **-** | **-** | **39,653** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.04.2023** | **21,500** | **-** | **16,231** | **585** | **-** | **-** | **38,317** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 694 | - | - | - | **694** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (835) | 835 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 108 | - | - | - | **108** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.06.2023** | **21,500** | **-** | **16,199** | **1,420** | **-** | **-** | **39,119** |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-23 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-22 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 669 | 829 | 1,664 | 1,356 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 673 | 642 | 2,413 | 1,644 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,009) | (5,562) | (4,800) | (14,294) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,577 | 5,488 | 11,288 | (4,310) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (5,475) | 2,527 | (3,814) | (196) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (48) | (739) | (645) | 432 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (173) | (411) | (466) | 80 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (135) | (135) | (404) | (560) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(4,921)*** | ***2,639*** | ***5,236*** | ***(15,848)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (6) | (1) | (7) | (284) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(6)*** | ***(1)*** | ***(7)*** | ***(284)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(4,927)** | **2,638** | **5,230** | **(16,132)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 34,085 | 31,447 | 23,928 | 45,094 |
| | **Mwaka** | **29,158** | **34,085** | **29,158** | **28,962** |

#### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Antaryami Sarangi<br>**Mkurugenzi Mkuu** | | 27.10.2023 |
| Mr. Mahadhil M.Karwani<br>**Mkuu wa Fedha** | | 27.10.2023 |
| Mr. Allen Richard<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | 27.10.2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi | | 27.10.2023 |
| 2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi | | 27.10.2023 |

176818



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akikata utepe katika uzinduzi wa Mradi wa Kufua Umeme Ijangala Kijiji cha Masisiwe, wilayani Makete, mkoani Njombe. Mradi huo umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo TIB, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na mashirika ya kimataifa ya UNIDO na UNCDF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hatifungani ya Kijani ya CRDB yaorodheshwa DSE

## -Ni baada ya kukusanya bilioni 170/-

**Na Mwandishi Wetu**

HATIFUNGANI ya Kijani ya Benki ya CRDB imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) baada ya kufanikiwa kukusanya Sh. bilioni 171.82 kufadhili miradi inayotunza mazingira.

Benki hiyo imetangaza matokeo ya mauzo ya hatifungani yake hiyo iliyoweka historia ya kuwa ya kwanza ya kijani nchini na kubwa zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara katika hafla iliyofanyika kwenye jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Hatifungani hiyo iliyozinduliwa Septemba Mosi mwaka huu na kufungwa Oktoba 6 mwaka huu, imekuwa na mwitikio mkubwa na hivyo kupelekea kufikia lengo kwa asilimia 429.57 ambapo jumla ya Sh. bilioni 171.82 zimekusanywa kulinganishwa na lengo la awali la Sh. bilioni 40. Kati ya wawekezaji 1,754 waliowekeza kwenye hatifungani hiyo, asilimia 99 ni Watanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kamishna wa Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha wa Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamaja, aliyekuwa mgeni rasmi akimwakilisha Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alipongeza Benki ya CRDB kwa ubunifu na juhudi ilizochukua kuitoa na kuiuza hatifungani hiyo.

Dk. Mwamaja alisema idadi kubwa ya wawekezaji waliojitokeza kuwekeza kwenye hatifungani hiyo inadhihirisha juhudi kubwa zilizofanywa na Benki ya CRDB na fedha zilizopatikana zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuchochea utekelezaji wa ajenda za maendeleo na juhudi za kulinda mazingira.

Kamishna Mwamaja pia alisisitiza umuhimu wa kulinda mazingira katika juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kwamba ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi si tu unahitajika, bali haukwepeki kwa kuwa mahitaji ni makubwa.

"Tanzania inahitaji takriban Dola bilioni 19.2 za Marekani mpaka mwaka 2030 (ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu) ili kutoa mchango wake unaohitajika katika vita dhidi ya uharibifu wa mazingira.

"Sehemu kubwa ya fedha hizi inatakiwa itolewe na sekta binafsi. Kwa niaba ya serikali, ninapenda ninawapongeze kwa juhudi mnazozifanya ikiwamo Hatifungani hii ya Kijani na nyinginezo kama vile Programu ya Matumizi ya Teknolojia Endelevu za Kilimo Tanzania (TACADTP) mnayoshirikiana na Mfuko wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNGCF)," alisema Dk. Mwamaja.

Akiwashukuru wawekezaji waliojitokeza kwa imani waliyonayo na ushirikiano walioutoa hata kuwezesha mauzo hayo kuvuka malengo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema kiasi kilichokusanywa kimeongeza mtaji mpya ndani ya taasisi hiyo kwa Sh. bilioni 140 zitakazochochea utoaji mikopo kwenye miradi inayolenga kulinda mazingira nchini.

Mikopo hiyo si tu itaongeza upatikanaji ajira hasa kwa vijana na kukuza uchumi, bali pia Nsekela alisema itadhihirisha utayari na umakini wa Tanzania kutunza mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

"Ongezeko hili la mtaji wa Benki yetu ya CRDB litatuwezesha kutoa fedha zinazohitajika kwenye miradi tofauti inayojihusisha na kutunza mazingira kama vile viwanda endelevu, nishati safi, ujenzi na usafirishaji, maji, afya na elimu. Ninawaomba wawekezaji wa ndani na kimataifa mwendelee kushirikiana na benki yetu kufanikisha miradi hii," alisema Nsekela.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, alipongeza Benki ya CRDB kwa mafanikio iliyoyapata na kusema Hatifungani hiyo ya Kijani imetolewa kwa muda mwafaka kukidhi mahitaji yaliyopo.

Baada ya matokeo hayo kutangazwa, Hatifungani ya Kijani ya CRDB iliorodheshwa rasmi DSE ili kuuzwa katika soko la upili.

Akizungumza wakati wa uorodheshaji wa hatifungani hiyo sokoni, Kaimu Ofisa Mtendaji wa Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE), Mary Mniwasa alisema mauzo ya Hatifungani ya Benki ya CRDB si tu yameinufaisha taasisi hiyo, bali pia soko zima la fedha nchini.

"Kuorodheshwa kwa 'Kijani Bond' kutakwenda kuongeza uuzaji na ununuaji dhamana katika soko hilo maradufu kutoka wastani wa sasa wa Sh. bilioni 150 hadi zaidi ya Sh. bilioni 300," alisema Mniwasa.

Mkuu wa Idara ya Uchumi katika Ubalozi wa Uingereza nchini, Euan Davidson, alisema Uingereza imefurahia kufanikisha kutolewa hata kuuzwa kwa Hatifungani ya Kijani ya Benki ya CRDB.

Mchango wa taifa hilo umetolewa kupitia Taasisi ya FSD Africa iliyokuwa mshauri huru katika mchakato mzima wa kutoa mpaka kuuzwa kwa Hatifungani ya Kijani.

Hayo yote yalifanyika yakiwezeshwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (UK Development).

"Historia iliyoandikwa katika mauzo ya hatifungani hii kwa wingi wa wawekezaji binafsi hata mashirika yanadhihirisha kukubalika kwa sekta ya fedha ya Tanzania na kuonesha kwamba kuna uhitaji mkubwa wa fedha za kufanikisha miradi ya mazingira mwongoni mwa wawekezaji tofauti wa ndani na kimataifa," alisema Davidson.

Shirika la IFC lililo chini ya Benki ya Dunia ni miongoni mwa wawekezaji waliotoa kiasi kikubwa kwenye mauzo ya hatifungani hiyo. Shirika hilo pekee limewekeza Sh. ambazo ni sawa na dola milioni 20 sawa na asilimia 29.3 ya uwekezaji wote uliofanyika.

Meneja wa Kanda ya Afrika Mashariki IFC, Jes Chonzi alisema: "Upatikanaji wa fedha za kufanikisha miradi inayolinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni fursa iliyo wazi kwa Tanzania na fedha nyingi zinahitajika hasa kutoka sekta binafsi.

"Hatifungani hii itaongeza upatikanaji wa mikopo kwenye miradi ya mazingira na kuongeza ujumuishaji wananchi katika uchumi."

Katika mchakato wa kutolewa na kuorodheshwa kwa 'Kijani Bond', Benki ya Stanbic Tanzania ilishiriki kama msimamizi mkuu, huku kampuni ya Denton Tanzania Law Chamber ikitoa huduma za ushauri wa kisheria. Kampuni ya Orbit Securities Tanzania ilikuwa wakala mfadhili, huku KPMG ikikabidhiwa majukumu ya kutoa taarifa za kihasibu.

'Kijani Bond' ni awamu ya kwanza ya mpango wa dhamana ya uwekezaji ya Benki ya CRDB wenye thamani ya Dola za marekani milioni 300 unaolenga kukusanya fedha kwa ajili ya ufadhili miradi ya kijani, kijamii na endelevu.

Benki hiyo imejitolea kuendeleza ukuaji wa uchumi wa kijani na shirikishi nchini kupitia ufadhili bunifu na rafiki kwa mazingira.

***TAZAMA PICHA ZA HAFLA YA UTANGAZAJI MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI HIYO UK. 5**

# Uondoshaji taka Dar pasua kichwa

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema tatizo la uondoshaji taka mkoani humo ni kubwa na kudumaza viwango vya usafi, hatua iliyoufanya mkoa kuunda kitengo maalumu cha ukusanyaji taka.

Alisema mfumo wa ukusanyaji taka utakabidhiwa kwa mkandarasi mmoja na si kama ilivyo sasa makandarasi tofauti kutumika kufanya shughuli hiyo mitaa tofauti, jambo linalosababisha kutokuwapo kwa ufanisi na ufuatiliaji wa majukumu yao.

Kadhalika, kuna usimamizi duni eneo la ukusanyaji taka katika dampo la Pugu Kinyamwezi, akikiri baadhi ya mafuta ya magari aina ya magreda kwa ajili kuendesha shughuli katika eneo hilo kuibwa.

Chalamila aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano Mkuu wa Klabu ya Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), huku akijibu hoja mbalimbali kutoka kwa wanachama wa klabu hiyo, baada ya kuwasilisha mafanikio na changamoto za mkoa huo.

Juni, mwaka huu, gazeti hili lilifika eneo la dampo la Pugu Kinyamwezi, Jiji la Dar es Salaam na kubaini kasoro kadhaa, kama kujaa kwa dampo, kutokuwapo kwa magari maalum (buldoza) ya kusambazia taka na utoroshwaji mafuta na malori yanayofikisha taka eneo hilo kukaa saa nyingi kwenye foleni.

Baadhi ya wafanyakazi binafsi wanaofanya kazi katika dampo hilo, ikiwamo madereva wa malori yanayowasilisha taka kwenye dampo hilo, walikiri ugumu wa kazi kutokana na foleni ndefu inayowalazimu kutumia siku nzima hadi kukamilisha kazi ya kumwaga taka.

"Pale kuna magreda yetu yanaiba mafuta. Tumepeleka watu wetu Seoul (Korea Kusini) kwenda kujua namna wanavyochakata taka. Kuna kitu kilishakosewa tangu mwanzo, mji tumeacha umejaa kwa kupeleka taka Pugu Kinyamwezi ni eneo moja na ni mbali," alisema Chalamila.

"Kuna risiti za mkononi na watu wanaingia hawakaguliwi. Mji ni mchafu 'Lets feel shame, ourselves' (tujusikie aibu wenyewe), mimi mwenyewe nilikuwa Seoul (Korea Kusini), inahitajika akili kubwa kuhusu taka."

Alisema kutokana na mkoa huo kubeba taswira ya nchi ikiwamo uwapo wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), kunahitajika uwekezaji na maboresho ya maeneo ya kufanyia utalii na kuongeza ujenzi wa hoteli zenye hadhi ya kimataifa.

Mkoa wa Dar es Salaam, unakadiriwa kuzalisha taka takribani tani 5,600 kwa siku huku asilimia 45 hadi 50 pekee ndizo hudhibitiwa na kupelekwa katika dampo la Pugu Kinyamwezi, linalotegemewa na mkoa mzima, kutoka wilaya tano za mkoani humo.

Mkoa una wilaya tano; Kigamboni, Ilala, Ubungo, Temeke na Kinondoni, kiwango cha uzalishaji taka hutofautiana, huku mzigo mkubwa ukiwa Halmashauri ya Ilala ambako taka zinapokewa katika dampo la Pugu Kinyamwezi.

Kukua kwa jiji na idadi kubwa ya wakazi inayofikia milioni 5.4 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022, kumeongeza changamoto ya uondoaji taka maeneo ya makazi, masoko na maofisini.

# BENKI YA CRDB YATANGAZA MATOKEO YA HATIFUNGANI YA KIJANI




MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA CRDB, ABDULMAJID NSEKELA AKIZUNGUMZA WAKATI WA HAFLA YA KUTANGAZA MATOKEO YA HATIFUNGANI YA KIJANI YA BENKI HIYO 'KIJAN BOND' ILIYOFANYIKA KATIKA HOTELI YA JOHARI ROTANA. KUPITIA KIJANI BOND BENKI YA CRDB IMEKUSANYA SHILINGI BILIONI 171.82 SAWA NA ASILIMIA 429.57 YA LENGO LA KUKUSANYA SHILINGI BILIONI 40 AMBAZO ZITAELEKEZWA KATIKA KUFADHILI BIASHARA NA MIRADI INAYOZINGATIA UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI.




MKURUGENZI WA MAWASILIANO BENKI YA CRDB, TULLY MWAMBAPA AKIELEZEA JUU YA UWEKEZAJI ULIOFANYIKA KATIKA KIJANI BONDI AMBAPO ASILIMIA 99 YA UWEKEZAJI UNATOKANA NA WAWEKEZAJI WA NDANI HUKU SHILINGI BILIONI 140 ZIKIWA NI FEDHA MPYA KATIKA MZUUNGUKO JAMBO AMBALO LITASAIDIA KUCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI KWA KIASI KUBWA.




VIONGOZI NA WAWEKEZAJI MBALIMBALI KATIKA HATIFUNGANI YA KIJANI YA BENKI YA CRDB 'KIJANI BOND' WAKIFUATILIA UTANGAZAJI WA MATOKEO YA HATIFUNGANI HIYO BAADA YA DIRISHA LA UWEKEZAJI KUFUNGWA TAREHE 6 OKTOBA 2023. HAFLA YA UTANGAZI MATOKEO HAYO ILIFANYIKA KATIKA HOTELI YA JOHARI ROTANA JIJINI DAR ES SALAAM.



KAMISHNA WA IDARA YA UENDELEZAJI SEKTA YA FEDHA KUTOKA WIZARA YA FEDHA, DKT CHARLES MWAMAJA (KATIKATI) AKIPIGA KENGELE KUASHIRIA KUORODHESHWA KWA HATIFUNGANI YA KIJANI YA BENKI YA CRDB KATIKA SOKO LA HISA DAR ES SALAAM (DSE). WAKISHUHUDIA TUKIO HILO NI KAIMU AFISA MTENDAJI WA SOKO LA HISA DAR ES SALAAM (DSE), MARY MNIWASA (WANNE KULIA), AFISA MTENDAJI MKUU WA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA), CPA NICODEMUS MKAMA (WATANO KULIA), MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA CRDB, ABDULMAJID NSEKELA (WATANO KUSHOTO), PAMOJA NA WAWEKEZAJI KATIKA HATIFUNGANI HIYO NA VIONGOZI WA BENKI YA CRDB.



KAMISHNA WA IDARA YA UENDELEZAJI SEKTA YA FEDHA KUTOKA WIZARA YA FEDHA, DKT CHARLES MWAMAJA (KUSHOTO) AKIFURAHIA JAMBO NA MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA CRDB, ABDULMAJID NSEKELA BAADA YA KUTANGAZWA KWA MATOKEO YA HATIFUNGANI YA KIJANI YA BENKI YA CRDB 'KIJANI BOND' AMBAPO SHILINGI BILIONI 171.82ZIMEKUSANYWA SAWA NA ASILIMIA 429.57 YA LENGO LA KUKUSANYA SHILINGI BILIONI 40.



MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA CRDB, ABDULMAJID NSEKELA AKISALIMIANA NA MKUU WA IDARA YA UCHUMI KATIKA UBALOZI WA UINGEREZA NCHINI, EUAN DAVIDSON. UINGEREZA NI MOJA YA WADAU AMBAO WAMESHIRIKI KATIKA KUFANIKISHA MAFANIKIO YA 'KIJANI BOND' KUPITIA TAASISI YA FSD AFRICA ILIYOKUWA MSHAURI HURU KATIKA MCHAKATO MZIMA WA KUTOA MPAKA KUUZWA KWA HATIFUNGANI HIYO YA KIJANI.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uwekezaji wa viwanja unahitajika kukuza utalii wa michezo nchini

**TANZANIA** kwa sasa imekuwa miongoni mwa nchi ambazo utalii wa michezo unaelekea kukua kwa kasi na muda si mrefu tunaamini sekta hiyo itachangia kiasi kikubwa katika pato la taifa kama utafanyika uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya viwanja.

Tumeshuhudia kwa miaka ya hivi karibuni hususan mwaka jana na huu, nchini za Ukanda wa Afrika na Mashariki na Kati, timu zao za taifa na klabu zikiomba kuchezea mechi zao za nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na ule wa Azam Complex uliopo Chamazi.

Timu hizo zimekuwa zikiomba kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa na Azam Complex, kutokana baadhi kutokuwa na viwanja vilivyokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), ama kwa sababu ya machafuko ya kisiasa nchini kwao.

Mfano ni TP Mazembe ya DR Congo, ambayo mechi yake ya nyumbani ya michuano African Football League wiki iliyopita ilichezwa kwa Mkapa kutokana na serikali yao kushindwa kulipia vifaa vilivyotakiwa kuingia nchini humo kwa ajili ya mchezo huo.

Lakini pia nchi za Burundi na Sudan Kusini mara kadhaa zimekuwa zikitumia viwanja hivyo kutokana na sababu tulizotaja hapo juu na zinginezo, hivyo kuingizia Serikali ya Tanzania kiasi kikubwa cha fedha za kigeni.

Kwa sasa, pia zipo taarifa ambazo bado hazijathibitishwa rasmi kuwa timu ya Al Hilal ya Sudan imeomba kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mechi zake tatu za nyumbani za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Al Hilal imefikia hatua hiyo kutokana na hali ya machafuko ya kisiasa inayoendelea nchini kwao Sudan na hata mechi za awali za michuano hiyo ilikuwa ikichezea nchini Morocco.

Na kwa mujibu wa Meneja Uwanja wa Benjamin Mkapa, Milinde Mahona, kuruhusiwa kucheza mchezo mmoja tu uwanjani hapo gharama yake ni Sh. milioni 20.

Mbali na kiasi hicho, ikumbukwe pia wageni kama hao wanapokuja nchini, wafanyabiashara mbalimbali kama wamiliki wa hoteli na biashara nyingine hunufaika, ikiwamo nchi kuingiza fedha za kigeni.


Tunaamini kama serikali na wadau wengine wa soka wakiwekeza zaidi katika miundombinu bora ya viwanja nchi itaingiza fedha nyingi zaidi za kigeni kupitia utalii wa michezo, kwani kwa sasa tunategemea uwanja mmoja tu, Benjamin Mkapa unaobeba watazamaji 60,000 na mara chache ule wa Azam Complex ambao uwezo wake ni mashabiki 10,000 tu.

Kwa kuwa kuelekea fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2027, zitakazofanyika kwa ushirikiano wa Tanzania, Kenya na Uganda, tayari serikali imepanga kujenga viwanja vingine bora viwili, jijini Arusha na Dodoma, vinapaswa kuwa vya kisasa zaidi vyenye sifa zote stahiki.

Lakini pia, bado tunaona ipo haja ya kujengwa uwanja mwingine wa kisasa jijini Dar es Salaam, pia uboreshwaji wa miondombinu ya barabara, hospitali kubwa na vifaa tiba vya kutosha ili kuvutia na baadaye kukuza utalii wa michezo nchini.

Tunaamini hayo yakitekelezwa na kwa namna Watanzania wanavyohamasika kujitokeza kwa wingi viwanjani katika mechi kubwa, ipo siku michuano mikubwa ama mechi kubwa za fainali zitapigwa nchini na Tanzania kuzidi kuingiza fedha nyingi za kigeni kupitia utalii wa michezo ambao unazidi kukua duniani kila uchao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# 'Zimwi' linaloitafuna Azam FC lisakwe

**KUNA** zimwi linaitafuna Klabu ya Azam na mpaka sasa hakuna yeyote anayefahamu linapoishi. Mashabiki na wadau wa soka wanaolitakia mema soka la Tanzania wamekuwa wakilitafuta huku na huko bila mafanikio.

Sina uhakika kama wenyewe Azam wamekaa kwa dhati kabisa kuangalia tatizo ni nini.

Na kama wanajua basi inaonekana kuna kuoneana haya kuisafisha klabu hiyo na kutengeneza safu nyingine ya viongozi, watendaji, ikiwezekana watoke hata nje ya nchi.

Azam ndiyo yenye miundombinu halisi inayotakiwa iwe nayo klabu ya mpira wa miguu. Hakuna klabu yoyote Tanzania yenye miundombimu kama Azam, hata zile kongwe zinazoitwa au kujiita kubwa za Simba na Yanga.

Lakini Azam hii hii ndiyo timu inayozifanya hata klabu hizo na wanachama na mashabiki wao zisione umuhimu huo kwa sababu kama wao wana kila kitu na hawafanyi vizuri, basi ni bora tu kufanya vizuri uwanjani kuliko kuwa na miundombinu ambayo haisaidii chochote.

Kabla sijasonga mbele, nikumbushe tu kuwa pamoja na kuonekana kusajili wachezaji bora na ghali msimu huu, tayari Azam FC, taratibu inaonekana kuanza kujitoa kwenye kinyang'anyiro cha ubingwa wa Tanzania Bara.

Imeshapoteza mechi mbili mfululizo ikipigwa mabao 3-2 dhidi ya Yanga na 3-1 dhidi ya Namungo, huku ligi ikiwa bado mbichi raundi ya nane.

Kila msimu ukiiangalia, Azam ni timu ambayo inaonekana kusajili vizuri zaidi kuliko zingine, lakini linapokuja suala la uwanjani mambo yanakuwa tofauti.

Tayari imeshatolewa mapema kwenye michuano ya kimataifa na jambo hilo limeonekana kuwakera sana mashabiki wake na baadhi ya wadau wa soka, ilitegemewa nguvu zote zitaelekezwa kwenye ligi, lakini inaonekana bado hawajapata mwarobaini kwa nini huwa inafeli.

Wachezaji mmoja mmoja wa Azam wana viwango vya juu na ukiwapeleka Klabu za Simba na Yanga baadhi yao wanaingia kwenye kikosi cha kwanza.

Huwezi kuniambia leo kuwa Feisal Salum na Yanick Bangala wakirudi Yanga hawapati namba. haiwezekani mchezaji kama Kipre Junior, Gilbril Sillah na James Akaminko wakienda Simba watakaa benchi, kuna watu watawapisha.

Sasa inakuwaje wakiwa Azam hawawezi kuibeba timu hiyo? Hilo ndilo swali linaulizwa. Zipo dhana kwa baadhi ya wadau wa soka kuwa Azam na wachezaji wake hukamia mechi kubwa tu za Simba na Yanga, lakini wakicheza na zingine wachezaji hawajitumi.

Dhana nyingine iliyojengeka ambazo zote inawezekana zina asilimia fulani za ukweli ni kwamba Azam haina mashabiki wa kaliba ya wale wa Simba na Yanga.

Hawana mashabiki wanaoumia kweli kutoka ndani ya mioyo yao. Ni mshabiki wa 'kununuliwa au kukodishwa' tu, hivyo hata ikifungwa hawaumii, tofauti na wa Simba na Yanga ambao hata zikitoka sare ya kizembe tu, uwanjani na kwenye mitandao ya kijamii kunachafuka maneno ya ukali wa mashabiki wao, hivyo kila mechi wachezaji wanajituma kwa ajili ya kufurahisha na kuwaogopa mashabiki.

Je, wamiliki wa timu hiyo wameshaangalia wapi wanapojikwaa? Je, wana nia ya dhati timu hiyo iwe bingwa wa Tanzania, au ipo kwa ajili ya kibiashara tu? Hilo ndilo swali linaloulizwa kwa sasa.

Azam ndiyo klabu inayofukuza makocha wengi kuliko zote na mpaka sasa imeshaonekana tatizo siyo hilo. Tatizo lipo ndani ya klabu yenyewe. Kama ni zimwi basi binafsi nadhani lipo kwenye moja ya vyumba vya klabu hiyo.

Kwa miaka yote hii timu inafanya usajili mzuri, lakini hata nafasi ya pili haipati licha ya kwamba kuna wakati Simba na Yanga hazipo vizuri, lakini yenyewe inaishia ya tatu. Nadhani hii haifanyiki kwa bahati mbaya, kuna tatizo.

Azam ni timu ya kuukosa ubingwa kwenye mechi tatu nne za mwisho na si mwanzo tu ionekane kusalimu amri. Zimwi yupo humo humo ndani, asakwe.

## HABARI KITAIFA

# Matinyi: Hakukuwa na usiri utiaji saini uwekezaji Bandari

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi (pichani), amesema hakukuwa na usiri katika utiaji saini wa uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Alitoa ufafanuzi huo jana wakati akijibu maswali katika mkutano wake na wahariri na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, kuwa kila kitu kilikuwa wazi.

"Kila mtu alizungumza, Rais alizungumza, Makamu na watu wa DP World walizungumza, kiukweli hapakuwa na usiri hata kama unaeleza umefika Dodoma hukujua umealikwa kwa kitu gani udai kulikuwa na usiri, lakini ulikiona kilichofanyika sidhani kama hiyo inatosha kusema jambo lilikuwa ni la siri wakati limewekwa wazi na kila mtu ameona," alisema.

Kuhusu mkataba wa wazawa na DP World, alisema mkataba umeeleza kutakuwa na kampuni itakayoundwa kati ya Mamlaka ya Bandari (TPA) na wawekezaji hao.

Alisema kampuni hiyo ya pamoja itakapoundwa itasajiliwa Tanzania na kazi yake ni kuendesha magati manne na muda utakapofika taratibu zitatangazwa kuhusu wazawa watahusika kwa namna gani kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema ubia uliowekwa kuhusiana na uwekezaji wa bandari, ipo haja ya Watanzania kufahamu kwa kuwaelimisha wajue fedha itakayokusanywa ni kodi za namna gani ama taasisi zilizopo.

Aidha, alisema katika makubaliano ya mkataba huo magati yataongezwa eneo la Kurasini na kumilikiwa na Bandari ya Dar es Salaam bila kuathiri nyumba za wananchi.

Aidha, alisema kitengo cha mafuta kilichopo eneo hilo kitaondolewa na kupelekwa eneo jingine la Kigamboni na ifikapo mwaka 2026 kutakuwa na magati 20.

"Huo ndio mpango uliopo na huenda yakongezeka kwa sababu biashara iliyopo kwenye nchi jirani ni kubwa," alisema.

Kadhalika, Matinyi alisema huhusu Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, waziri anayehusika amemjulisha atahusisha wadau wa sekta ya habari na utaratibu umepangwa watapatiwa barua na rasimu ya kanuni ili wazipitie na kutoa maoni yao Novemba 10, mwaka huu wayawasilishe.

Alisema Novemba Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, atakutana na wadau kujadiliana na kusikia maoni yao kulingana na ratiba huenda ikawa Novemba 18 au 19, kuwasikiliza kabla ya kwenda kukamilisha kanuni.

Matinyi alisema Sheria hiyo inatamka kwamba itaundwa bodi ya ithibati ya waandishi wa habari na tayari wameshaomba majina ya vyombo vya habari mchakato unaweza kukamilika Desemba, mwaka huu.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na vyombo vya habari inahakikisha wananchi wanapata taarifa japo kumekuwa na changamoto kwa pande zote.

"Nakubali kwamba kupata taarifa kutoka kwenye chombo cha serikali ama wizara wakati mwingine inakuwa ni ngumu hilo nalikubali na pia ukizungumza na watendaji serikali wanakuambia nilitoa taarifa ikatolewa tofauti na nilivyoitoa nikapata usumbufu wanakuwa na hofu," alisema.

Akizungumza hali inayoendelea nchini Israel, alisema hali ni ngumu kwa sababu kuna vijana wa Kitanzania ambao wanasoma huko.

"Tunafuatilia kupitia ubalozi wetu ili kufahamu hali zao na kuona ni namna gani tunaweza kuwasaidia, hivyo serikali inalifuatilia jambo hilo kwa ukaribu na tutakuwa tunaendelea kuwapatia taarifa unaposikia kuna Mtanzania amepotea ni lazima tujiridhishe kwamba amepotea kwa maana gani katika mvurugano wa vita anaweza kuchukua maamuzi ya kujilinda na kuamua kujificha itakapothibitika tutawapa taarifa," alisema.



Matinyi alimpongeza Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ziara aliyoifanya Zambia kutokana na nchi hiyo kuwa na historia ya muda mrefu katika kukuza uchumi.

Pia, anampongeza Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwa kushinda nafasi ya kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge duniani na kuwa mwanamke wa kwanza Afrika kushika nafasi hiyo.

# Canada yaipatia Tanzania bil. 45/- fursa elimu jumuishi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Canada imetoa msaada wa Sh. bilioni 45 zitakazotumika kuboresha fursa za elimu jumuishi kwa vyuo vya maendeleo ya jamii katika kipindi cha miaka saba.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitoa shukrani kwa msaada huo katika hafla ya makabidhiano ya vifaa vya TEHAMA kwa FDCs 12 (Vyuo vya Maendeleo ya Jamii) na CBOs 12 (Taasisi za Kijamii) Ofisi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Waziri, Omari Kipanga kwa niaba yake, alisema msaada huo umekuja wakati Tanzania inapitia mabadiliko makubwa ya sera ya elimu.

Aliishukuru Canada kwa msaada huo na kuomba zaidi kufikia FDCs 42 zilizobaki ambazo hazijashughulikiwa.

Programu inayotekelezwa na vyuo na taasisi za Canada (CICan) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Tanzania na kufadhiliwa na Serikali ya Canada ni Sh. bilioni 1.8 kati ya hizo, zimetengwa kwa ajili ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Hellen Fytche, Mkuu wa Ushirikiano, ubalozi wa Canada nchini wakati akikabidhi vifaa hivyo alisema, lengo kuu ni kuboresha ushiriki wa wanawake na vijana wa kike kiuchumi kwa kutoa njia mbadala za elimu na kukuza ujuzi kwa ajira, kujiajiri, na ujasiriamali.

Alisema Canada imefurahishwa na hatua iliyofikiwa na Tanzania katika kuboresha sekta ya elimu; msaada huo unalenga kukamilisha kazi nzuri ya Serikali ya Tanzania.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alisema Mpango wa Uwezeshaji kupitia ujuzi ulifanya tathmini ya awali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kubaini upungufu wa uwezo katika FDCs 12 na CBO 12.

Alisema matokeo yalionyesha hitaji kubwa la kubadilisha mazingira ya ufundishaji, ujifunzaji na utawala katika FDCs zote 12 na CBOs 12.

Alisema kila FDC itapokea vishikwambi vitatu, kompyuta nne za mezani, projekta moja ya media titika, printa mbili zinazofanya kazi nyingi na mfumo mmoja wa PA.

CBO zote 12 zitapokea kompyuta ndogo moja, projekta moja ya media titika, printa moja yenye kazi nyingi na mfumo mmoja wa PA.

Mshauri Mwandamizi wa Kiufundi wa ESP na Mwakilishi wa CICan nchini Tanzania, Dk. Alice Mumbi alisema, CICan ESP inaishukuru wizara kwa kufanya hesabu na kuweka alama za mali za vifaa vyote vya TEHAMA na kusajili maelezo yote katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS).

CICan pia ilishukuru Serikali ya Tanzania kwa kupunguza asilimia 18 ya VAT, ambayo iliwezesha ESP kununua vifaa zaidi vya teknolojia kwa wafanyakazi na wanafunzi wa FDC, CBOs, na wanufaika wengine wa mradi ambao watafaidika na mabadiliko ya mazingira ya kufundishia, kujifunzia na kiutawala.

Kabla ya awamu ya pili ya ununuzi wa ICT, ESP itatathmini miundombinu ya FDCs 12 na kutoa mapendekezo ya mpangilio wa ICT kwa vitovu vya uvumbuzi, warsha na madarasa.

Katika maandalizi, ESP itawafunza wafanyakazi wote katika FDCs washirika na CBOs juu ya ujuzi muhimu wa kompyuta.


TANZANIA INVESTMENT CENTRE — THE FACILITATOR

**KITUO CHA UWEKEZAJI WA TANZANIA (TIC)**

**MWALIKO WA KUSHIRIKI KONGAMANO LA BIASHARA NA UWEKEZAJI BAINA YA TANZANIA NA UHOLANZI**

Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Uholanzi wanaandaa Kongamano la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Uholanzi litakalofanyika kuanzia tarehe 14 hadi 15 Novemba 2023 Jijini The Hague, Uholanzi. Kongamano hili limelenga kutangaza fursa za uwekezaji na biashara zilizopo katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Nishati, Ujenzi na Miundombinu

Programu ya Kongamano hili itajumuisha mikutano ya kibiashara pamoja na kutembelea maeneo ya viwanda vilivyopo nchini Uholanzi katika sekta zilizolengwa ili kujifunza zaidi kutoka kwa wenzetu nchini Uholanzi

Hakuna gharama yeyote ya kushiriki Kongamano hili, aidha, kila mshiriki atajigharamia usafiri na malazi. Karibu ujisajili kwa kupitia mawasiliano yafuatayo;

**Elizabeth Muzo +255 712 461232. Email elizabeth.muzo2@tic.go.tz**
**Benson Nkini +255 715 923 777, Email benson.nkini@tic.go.tz**

176814



# Kikwete kuongoza Kongamano la Kimataifa Uwekezaji na Biashara

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete (pichani) anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Kongamano la Kimataifa la Kujadili Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji na Biashara litakalofanyika jijini Dodoma mwezi ujao.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kuwa kongamano hilo litashirikisha wadau mbalimbali kutoka sekta zote nchini, serikali na taasisi zake.

Alisema kongamano hilo pia litawashirikisha wanataaluma kutoka vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi pamoja wadau kutoka sekta binafsi.

Prof. Edda alisema kongamano hilo pia litakuwa na mjadala kuhusu changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wafanyabiashara ili zitatuliwe na kupitia utafiti mbalimbali zilizofanywa na taasisi nyingine za utafiti.

Alisema kongamano hilo litakuwa na umuhimu na tija kubwa katika biashara kwa kuwa litashirikisha wafanyabiashara kutoka Finland, Japan, China, Uganda, Afrika Kusini na zingine jirani.

Alisema CBE imejipanga vyema kuhakikisha kongamano hilo linakwenda kujadili changamoto na mafanikio ya uwekezaji, biashara na kutoa majibu yatakayosaidia kuboresha shughuli za kiuchumi.

Pia alipongeza jitihada mbalimbali za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Alisema ziara za Rais Samia katika nchi mbalimbali ambazo amekuwa anazifanya, zimekuwa na mchango mkubwa katika kutangaza fursa za uwekezaji nchini.

Alisema ziara katika nchi mbalimbali kama vile Dubai, India, Zambia na Kenya ni moja ya jitihada muhimu ambazo zinafanywa na serikali katika kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini.

Prof. Edda alisema CBE inalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kutangaza na kuuza sekta ya utalii kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour, chuo hicho kikijikita katika kuhakikisha kinazalishia wataalamu wa biashara watakaoongeza mchango wa sekta ya biashara katika kukuza utalii nchini.

# 'Serikali ipunguze kodi na tozo kwenye korosho'

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimependekeza kupunguzwa kwa kinachoitwa utitiri wa kodi, ushuru na tozo kwenye korosho kwa Sh. 415 ili kumnusuru mkulima.

Pia kimeishauri serikali ipeleke muswada bungeni kupunguza makato ya ushuru wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka asilimia 15 hadi tisa.

Msemaji wa Sekta ya Kilimo, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa chama hicho, Mtutura Abdallah, alipendekeza hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu changamoto zinazolikabili zao la korosho nchini.

Viongozi wengine waliohudhuria mkutano huo ni Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Lindi, Isihaka Mchinjita na Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Mtwara, Alphonce Hittu.

Akisoma mapendekezo, Mtutura alisema hali ya mwenendo wa soko la korosho ikiachwa iendelee itapunguza kipato cha wakulima na kuwaingiza kwenye ufukara.

"Serikali itoe ruzuku ya kufidia soko la korosho ya Sh. 200 kwa kila kilo moja kama ilivyofanya kwenye mahindi huko Songea mwaka 2021/22 wakati soko lilipoyumba ili kumwokoa mkulima," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inapaswa itunge haraka sheria ya sekta ya kilimo ambayo itasaidia kudhibiti makundi ya viongozi mbalimbali kujipangia tozo wazitakazo kwa mazao ya kilimo, ikiwamo korosho.

Alisema serikali pia iachane na utaratibu wa soko la awali, kwamba kampuni zote zinazotaka kununua korosho zitumie utaratibu wa minadi.

Vilevile, alisema serikali inapaswa kutoa vivutio kwa kampuni zinazonunua korosho kwa ajili ya kubangua ndani ya nchi.

"Pili, kampuni zitakazopewa vivutio zipewe kibali cha kununua korosho kwa kiwango kinachoshabihiana na uwezo wa viwanda vyao vya kubangua korosho kwa mwaka," alisema Mtutura.

Kuhusu matumizi ya Bandari ya Mtwara, alisema: "Serikali iruhusu kutumika Bandari ya Dar es Salaam wakati mchakato wa kukamilisha ushoroba wa Mtwara ukiendelea."

Alisema serikali ipitie upya uamuzi wake na kwa haraka kujenga bandari kavu kwa ajili ya kujazia na kupakia magunia ya korosho na kuweka vivutio vya kuanzisha viwanda vya kubangua korosho nchini.

## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2023 | Robo Mwaka iliopita 30 Juni 2023 |
|---|---|---|---|---|
| A | | MALI | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 315.63 | 713.63 |
| | 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 9,787.52 | 5,387.60 |
| | 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 37,814.22 | 36,721.28 |
| | 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 687.01 | 1,373.88 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 25.99 | 100.10 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 3,989.91 | 7,641.61 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 47,709.24 | 50,836.69 |
| | 12 | Mali Nyingine | 1,974.01 | 1,677.66 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 863.40 | 959.44 |
| | 16 | **JUMLA YA MALI** | **103,166.91** | **105,411.89** |
| B | | DHIMA | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,247.00 | 8,207.50 |
| | 18 | Amana za Wateja | 58,280.42 | 53,867.90 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 | Amana Maalumu | - | - |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,726.46 | 1,609.81 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 | Dhima Nyingine | 675.05 | 669.79 |
| | 28 | Madeni | - | - |
| | 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **61,928.94** | **64,355.00** |
| | 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **41,237.98** | **41,056.90** |
| C | | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 190.10 | 557.45 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,457.61 | 7,254.41 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 760.27 | 415.04 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,237.98** | **41,056.90** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 6,738.45 | 6,886.70 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 120.32 | 669.25 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 153.61 | 204.41 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 39.97% | 38.95% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.25% | 1.31% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80.35% | 82.20% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 46.24% | 48.23% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87.43% | 91.62% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | -4.10% | -5.75% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -2.13% | -3.56% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2023 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Septemba 2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2023 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,243.10 | 2,079.17 | 6,477.12 | 6,667.88 |
| 2 | Gharama za Riba | 727.72 | 851.73 | 2,323.33 | 2,536.19 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,515.39** | **1,227.43** | **4,153.80** | **4,131.69** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 258.71 | - | 258.71 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (48.18) | 14.41 | 75.57 | 3.16 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **126.91** | **140.15** | **428.69** | **463.59** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2.64 | 24.19 | 85.57 | 141.63 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 124.27 | 115.96 | 343.13 | 321.96 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | !"#$%& - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **959.13** | **916.84** | **2,920.53** | **2,849.82** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 383.34 | 389.05 | 1,180.69 | 1,239.45 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 6.66 | 9.53 | 18.24 | 21.29 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 569.13 | 518.27 | 1,721.61 | 1,589.07 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **472.63** | **436.33** | **1,327.67** | **1,742.31** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 127.40 | 114.06 | 567.40 | 647.40 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **345.23** | **322.26** | **760.27** | **1,094.91** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 25 | 24 | 25 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 11 | 10 | 23 | 33 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 11 | 10 | 23 | 33 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.36% | 1.12% | 0.95% | 1.19% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.36% | 3.15% | 2.47% | 3.57% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 58.40% | 67.04% | 63.73% | 62.02% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.71% | 4.61% | 5.74% | 4.89% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2023 | Robo Mwaka iliopita 30 Juni 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2023 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2022 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 345.23 | 136.62 | 760.27 | 1,094.91 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 96.05 | 96.03 | 288.05 | (119.13) |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 3,127.45 | 2,591.13 | 2,335.94 | 3,491.20 |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | (2,547.98) | (3,789.20) | (3,791.31) | (29,057.44) |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 332.90 | (11.26) | 634.78 | 1,040.87 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (718.28) | (526.65) | (1,029.91) | (95.21) |
| Kodi iliyolipwa | (127.40) | (155.00) | (567.40) | (647.40) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **507.98** | **(1,658.32)** | **(1,369.58)** | **(24,292.19)** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (0.00) | (1.54) | (2.09) | 312.89 |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 2,720.78 | (1,988.09) | 6,286.00 | (7,770.60) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **2,720.78** | **(1,989.63)** | **6,283.91** | **(7,457.71)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | (164.15) | - | (164.15) | (492.45) |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (67.97) | (66.32) | (216.55) | (207.78) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(232.12)** | **(66.32)** | **(380.70)** | **(700.23)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 2,996.63 | (3,714.26) | 4,533.63 | (32,450.13) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 13,622.97 | 17,337.24 | 12,085.98 | 47,101.31 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **16,619.61** | **13,622.97** | **16,619.61** | **14,651.18** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/09/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 760.27 | - | - | - | **760.27** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (164.15) | - | - | - | **(164.15)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 277.60 | (277.60) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **8,217.88** | **190.10** | **-** | **-** | **41,237.98** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 895.43 | - | - | - | **895.43** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 811.68 | (811.68) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 25-10-2023 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 25-10-2023 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 25-10-2023 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 25-10-2023 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 25-10-2023 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

# TANGAZO

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

## "EXIM AT WORK TODAY, FOR TOMORROW"

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

## EXIM BANK (TANZANIA) UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA AMBAZO HAZIJAKAGULIWA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014.**

**Faida ya uendeshaji**
25.3% YoY
65.80 Bilioni

**Faida baada ya kodi**
1.7% YoY
41.00 Bilioni

**Mapato Halisi ya Riba**
14.0% YoY
105.70 Bilioni

**Amana za Wateja**
26.44% YoY
2.2 Trilioni

**Fedha za Wanahisa**
23.90% YoY
291 Bilioni

**Mapato Yasiyofadhiliwa**
5.1% YoY
77.80 Bilioni

**Mikopo na maendeleo**
19.66% YoY
1.4 Trilioni

**Jumla ya Mali**
17.65% YoY
2.9 Trilioni

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2023 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KAMPUNI ROBO MWAKA YA SASA 30.09.2023 | KUNDI ROBO MWAKA YA SASA 30.09.2023 | KAMPUNI ROBO MWAKA ILIY OPITA 30.06.2023 | KUNDI ROBO MWAKA ILIY OPITA 30.06.2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| A | MALI | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 29,739 | 60,982 | 43,340 | 72,034 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 101,336 | 182,528 | 99,985 | 171,653 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 420,150 | 502,769 | 386,185 | 461,656 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 203,418 | 504,316 | 50,068 | 244,887 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 1,590 | 8,771 | 2,183 | 3,474 |
| 6 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 68,306 | 68,423 | 67,324 | 67,496 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyigine | 2,787 | 2,079 | 723 | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 839,371 | 1,363,911 | 798,129 | 1,283,301 |
| 12 | Mali nyingine | 59,773 | 85,230 | 36,234 | 56,882 |
| 13 | Uwekezaji katika Hisa | 47,594 | 2,082 | 47,594 | 2,082 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 51,644 | 74,329 | 49,834 | 71,677 |
| 16 | Mali isiyo ya sasa inayotumiwa | - | - | - | - |
| 17 | JUMLA YA MALI | 1,825,707 | 2,855,421 | 1,581,599 | 2,435,142 |
| B | DHIMA | | | | |
| 18 | Amana za Benki na Taasisi za Fedha | 207,903 | 137,940 | 137,231 | 74,414 |
| 19 | Amana za Wateja | 1,274,547 | 2,218,524 | 1,125,473 | 1,949,687 |
| 20 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| 21 | Amana Maalumu | 8,790 | 13,465 | 10,648 | 16,131 |
| 22 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 23 | Hundi na Hawala za Kibenk Zilitolewa | 1,072 | 1,247 | 1,154 | 1,301 |
| 24 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 11,391 | 16,469 | 8,517 | 12,484 |
| 25 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya benki | - | - | - | - |
| 26 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 27 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 3,298 | 5,212 | 4,070 | 5,224 |
| 28 | Dhima Nyingine | 40,639 | 108,529 | 18,822 | 33,261 |
| 29 | Madeni | 43,278 | 43,278 | 51,481 | 51,481 |
| 30 | JUMLA YA D HIMA | 1,590,918 | 2,544,663 | 1,357,397 | 2,143,983 |
| 31 | MALI/(D HIMA) HALISI (17 kutoa 30) | 234,789 | 310,758 | 224,202 | 291,159 |
| C | FEDHA ZA WANA HISA | | | | |
| 32 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 12,900 | 12,900 | 12,900 | 12,900 |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 16,243 | 35,774 | 23,783 | 39,010 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | 177,304 | 201,324 | 170,692 | 197,365 |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 28,341 | 41,978 | 16,827 | 23,251 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - | - | - |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | 18,782 | - | 18,632 |
| 38 | JUMLA YA FEDHA ZA WANA HISA | 234,789 | 310,758 | 224,202 | 291,159 |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | 403,364 | 403,364 | 274,434 | 274,434 |
| 40 | Mikopo Chechefu | 93,430 | 122,730 | 124,887 | 176,352 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 39,657 | 47,982 | 41,711 | 50,109 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - | - | - |
| D | BAAD HI YA VIAS HIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | | | |
| | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.86% | 10.88% | 14.18% | 11.96% |
| | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 10.55% | 8.64% | 14.72% | 13.12% |
| | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 73.19% | 67.01% | 82.01% | 74.87% |
| | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 45.98% | 47.77% | 50.46% | 52.70% |
| | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.63% | 85.58% | 85.36% | 84.57% |
| | Ongezeko la Amana | 25.10% | 22.20% | 10.46% | 7.39% |
| | Ongezeko la Mali | 14.57% | 19.69% | -0.74% | 0.84% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2023 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KAMPUNI ROBO YA MWAKA YA SASA 30.09.2023 | KUNDI ROBO YA MWAKA YA SASA 30.09.2023 | KAMPUNI ROBO YA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.09.2022 | KUNDI ROBO YA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.09.2022 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2023 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2023 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.09.2022 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI (MWAKA ULIOPITA) 30.09.2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 35,175 | 53,052 | 29,951 | 43,761 | 97,227 | 142,496 | 85,381 | 124,392 |
| 2 | Gharama za Riba | (11,550) | (13,620) | (9,818) | (11,517) | (31,260) | (36,828) | (27,039) | (31,706) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 23,625 | 39,432 | 20,134 | 32,244 | 65,967 | 105,668 | 58,343 | 92,686 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | - | (1) | (1) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,111) | (3,582) | (13,287) | (14,018) | (832) | (5,604) | (10,450) | (13,042) |
| 6 | Mapato Yasi yo ya Riba: | 22,952 | 32,478 | 29,845 | 37,712 | 50,894 | 77,790 | 49,771 | 73,965 |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 13,117 | 15,387 | 3,090 | 5,509 | 25,345 | 31,677 | 7,881 | 14,380 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 8,046 | 15,037 | 6,527 | 12,189 | 20,387 | 40,325 | 16,444 | 33,280 |
| | 6.3 Gawio | 40 | 40 | - | - | 40 | 40 | 530 | 530 |
| | **6.4 Mapato Mengine** | **1,749** | **2,014** | **20,229** | **20,014** | **5,121** | **5,748** | **24,917** | **25,775** |
| 7 | Gha rama Zisi zo za Riba: | (25,448) | (39,100) | (22,604) | (34,747) | (70,184) | (112,050) | (65,907) | (101,138) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (12,381) | (19,004) | (10,277) | (15,575) | (33,808) | (52,834) | (29,080) | (44,526) |
| | **7.2 Ada na Kamisheni** | **(19)** | **(276)** | (44) | **(316)** | **(62)** | **(833)** | **(52)** | **(705)** |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (13,048) | (19,820) | (12,284) | (18,856) | (36,314) | (58,383) | (36,775) | (55,907) |
| 8 | Faida /(Hasa ra) ya Uen deshaji | 19,017 | 29,228 | 14,089 | 21,191 | 45,845 | 65,804 | 31,756 | 52,470 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (7,503) | (10,351) | (1,565) | (3,607) | (17,504) | (24,832) | (6,532) | (12,202) |
| 10 | Faida / (Hasa ra) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 11,515 | 18,876 | 12,523 | 17,583 | 28,341 | 40,972 | 25,225 | 40,268 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyo-jumuishwa (bainisha) | (928) | (3,021) | 16,887 | 13,059 | (4,051) | (3,021) | 16,879 | 21,005 |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | 10,587 | 15,855 | 29,411 | 30,642 | 24,290 | 37,950 | 42,104 | 61,273 |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 698 | 1,088 | 587 | 945 | 639 | 1,034 | 587 | 945 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 2,197 | 3,176 | 1,955 | 3,122 | 2,197 | 3,176 | 1,955 | 3,122 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 30 | 46 | 30 | 46 | 30 | 46 | 30 | 46 |
| | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | | | | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.7% | 2.9% | 1.2% | 1.7% | 2.2% | 2.1% | 1.8% | 2.0% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 20.7% | 26.3% | 9.6% | 17.3% | 17.0% | 19.0% | 14.3% | 20.7% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 53.7% | 56.8% | 68.4% | 64.2% | 53.6% | 56.7% | 63.1% | 61.9% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.3% | 8.2% | 7.7% | 8.0% | 6.8% | 7.4% | 1.8% | 1.9% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.09.2023 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KAMPUNI ROBO YA MWAKA SASA 30.09.2023 | KUNDI ROBO YA MWAKA SASA 30.09.2023 | KAMPUNI ROBO MWAKA ILIYO PITA 30.06.2023 | KUNDI ROBO MWAKA ILIYO PITA 30.06.2023 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2023 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2023 | KAMPUNI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.09.2022 | KUNDI LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.09.2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| I | Mtiriri ko wa Fedha Kutokana na S hughuli za Uendeshaji: | | | | | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 19,017 | 29,228 | 13,134 | 17,034 | 45,845 | 65,804 | 31,756 | 52,470 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| | Hasara Katika Mali | (2,111) | (3,582) | (1,434) | (3,151) | (832) | (5,604) | (10,451) | (13,043) |
| | Kushuka kwa Thamani na upungufu wa madeni | 2,831 | 5,704 | 2,426 | 4,206 | 7,650 | 13,253 | 8,454 | 13,365 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (41,242) | (80,610) | (55,161) | (41,670) | (76,663) | (116,150) | (83,730) | (108,266) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Net Gain/Loss on disposal of AFS | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 217,887 | 329,697 | 28,502 | 63,457 | 222,275 | 342,862 | 227,026 | 37,067 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | | | | | | | | |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 27,156 | 75,941 | (2,699) | (52,381) | 25,860 | (9,708) | 12,641 | 1,063 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (38,972) | (45,088) | (8,985) | (7,675) | (33,607) | (39,727) | (13,888) | 46,561 |
| | Non-current assets held for sale | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Kodi Iliyolipwa | (3,241) | (3,241) | (3,241) | (3,241) | (9,723) | (9,723) | (8,690) | (8,690) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Fedha Hali si zilizotolewa (zili zotumika) kw a shughuli za uendeshaji | 181,325 | 308,048 | (27,457) | (23,422) | 180,505 | 241,007 | 163,118 | 20,528 |
| II | Mtiriri ko wa Fedha Kuto kana na Shu ghuli za Uwekezaji: | | | | | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,436) | (2,436) | (2,564) | (2,564) | (9,291) | (9,291) | (6,660) | (6,660) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | (162,777) | (197,016) |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (36,029) | (43,192) | - | 65,906 | (15,947) | 43,110 | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshu-ghulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Fedha Hali si Zili zotol ewa (zili zot umika) kwa Shu ghuli za Uwe kezaji | (38,465) | (45,628) | 61,135 | **127,041** | (25,238) | 33,819 | (169,437) | (203,676) |
| III | Mtiriri ko wa Fedha Kuto kana na Shu ghul i za Ki fedha: | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (8,203) | (8,203) | 1,104 | 1,104 | (20,610) | (20,610) | (18,932) | (18,932) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha: | (8,203) | (8,203) | 1,104 | 1,104 | (20,610) | (20,610) | (18,932) | (18,932) |
| IV | Fedha Taslimu na Mali Zina zofanana na Fe dha Tasli mu: | | | | | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 134,657 | 254,217 | 34,782 | 104,723 | 134,657 | 254,217 | (25,250) | (202,080) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 191,817 | 427,937 | 157,035 | 323,213 | 191,817 | 427,937 | 166,869 | 503,540 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 326,474 | 682,154 | 191,817 | 427,937 | 326,474 | 682,154 | 141,620 | 301,461 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2023 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| KAMPUNI | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | "Mengine yo (bainisha)" | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 12,900 | 178,943 | 6,433 | 4 | 12,217 | 210,497 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 28,341 | - | - | - | 28,341 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | (4,051) | (4,051) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | (1,640) | 1,640 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 12,900 | 205,645 | 8,073 | 4 | 8,166 | 234,789 |
| Mwaka Uliopita | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 12,900 | 134,831 | 22,554 | 4 | 554 | 170,843 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 27,991 | - | - | - | 27,991 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | 11,663 | 11,663 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | 16,121 | (16,121) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 12,900 | 178,943 | 6,433 | 4 | 12,217 | 210,497 |

| KUNDI | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla na mengineyo | Maslahi Yasiyodhibiti | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa | | | | | | |
| Salio la mwan zo wa mwaka | 12,900 | 196,252 | 14,177 | 21,373 | 19,788 | 264,490 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 41,978 | - | - | (1,006) | 40,972 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | 5,296 | - | (5,296) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | 5,072 | (5,072) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 12,900 | 243,302 | 9,105 | 26,669 | 18,782 | 310,758 |
| Mwaka Uliopita | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 12,900 | 142,574 | 25,844 | 11,874 | 10,823 | 204,015 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 42,589 | - | - | 1,504 | 44,093 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | 8,921 | (8) | 8,913 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | 11,667 | (11,667) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | (578) | - | 578 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 12,900 | 196,252 | 14,177 | 21,373 | 19,788 | 264,490 |

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| JAFFARI MATUNDU<br>OFISA MTENDAJI MKUU | ................................... | 27.10.2023 |
| SHANI KINSWAGA<br>MKUU WA FEDHA | ................................... | 27.10.2023 |
| COLMAN RIWA<br>MKAGUZI MKUU WA NDANI | ................................... | 27.10.2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| SAID ALLY MWEMA<br>MWENYEKITI | ................................... | 27.10.2023 |
TAASISI YA KUTHIBITI UBORA WA MBEGU TANZANIA

TOSCI

TANZANIA OFFICIAL SEED CERTIFICATION INSTITUTE

**Kumb. Na.: AB. 136/441/01/36** **20/10/2023**

**Kwa: Wafanyabiashara ya Mbegu,**
**Tanzania Bara.**

## YAH: TAARIFA KUHUSU BEI ELEKEZI ZA MBEGU ZA MAHINDI ZINAZOUZWA KWA WAKULIMA

**Rejea kichwa cha habari hapo juu.**

2. Kama mtakavyokumbuka, tarehe 15 Oktoba 2023 Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein M. Bashe akiwa kwenye mkutano wa hadhara katika ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mkoani Manyara, alitoa maelekezo kwa TOSCI kutangaza bei elekezi ya mbegu za mahindi kufuatia malalamiko ya wananchi kuwa wamekuwa wakiuziwa mbegu hizo kwa bei ya juu na bei hizo zimekuwa zikibadilika mara kwa mara.
3. Baada ya kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo uwezo wa wakulima kununua mbegu na gharama za makampuni kuzalisha au kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi, Waziri wa Kilimo ameelekeza bei elekezi iwe kama ifuatavyo:

**Bei elekezi kwa mbegu za mahindi**
Bei elekezi ya mbegu za mahindi kwa msimu wa kilimo wa 2023/2024 itakuwa kama ifuatavyo:

i. **Aina za mbegu zinazochavushwa huria (Open Pollinated Varieties – OPVs)**
Bei elekezi kwa mbegu za aina zinazochavushwa huria itakuwa **4,000/=** kwa kilo moja au **8,000/=** kwa kifungashio cha kilo mbili.

ii. **Aina za mbegu chotara (Hybrid Varieties), zinazokomaa mapema na muda wa kati**
Bei elekezi kwa mbegu za aina chotara zinazokomaa mapema au muda wa kati itakuwa **7,150/=** kwa kilo moja au **14,300/=** kwa kifungashio cha kilo mbili.

iii. **Aina za mbegu chotara (Hybrid Varieties), zinazokomaa kwa muda mrefu**
Bei elekezi kwa mbegu za aina chotara zinazokomaa kwa muda mrefu itakuwa **8,000/=** kwa kilo moja au **16,000/=** kwa kifungashio cha kilo mbili.

iv. Bei elekezi za mbegu chotara zinazokomaa kwa muda mfupi na zinazokomaa kwa muda mrefu zinatofautiana kutokana na gharama kubwa inayotumika kupata mbegu za vizazi kwa ajili ya uzalishaji wa aina ya mbegu chotara zinazokomaa kwa muda mrefu.

4. Ili kuhakikisha kuwa wakulima wanauziwa mbegu kwa bei isiyozidi viwango elekezi, Waziri ameyataka makampuni kuwaelekeza mawakala wao wanaowauzia wakulima kutokuuza mbegu kwa zaidi ya bei elekezi na pia ameelekeza vyombo vya Serikali vitahakikisha mwongozo huu unazingatiwa kikamilifu.

**Bei elekezi kwa mbegu za mazao mengine**
Bei elekezi ya mbegu za mazao mengine zitaendelea kutolewa kadiri mahitaji yatakavyojitokeza.

5. Nawatakia utekelezaji mwema na ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Patrick Ngwediagi
**MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:**
**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Kilimo,**
**Mji wa Serikali Mtumba,**
**DODOMA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**TASTA,**
**ARUSHA.**

TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED - UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.09.2023

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014.

UBA United Bank for Africa

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | A. MALI | Robo Mwaka ya 30-Sep-23 | Robo Mwaka ya 30-Jun-23 |
|---|---|---|---|
| 1 | Fedha taslimu | 4,580 | 4,904 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 15,501 | 16,120 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za Serikali | 89,918 | 88,392 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | - | - |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | 1 |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 61,765 | 73,698 |
| 12 | Mali nyingine | 72,021 | 118,356 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika, mitambo na vifaa | 6,960 | 5,159 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **250,744** | **306,630** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | 56,523 | 64,965 |
| 18 | Amana za wateja | 145,889 | 195,774 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana maalumu | 5,596 | 7,941 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la kodi na gharama zitakazolipwa | 1,449 | 1,239 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 2,006 | 2,781 |
| 27 | Dhima nyingine | 6,729 | 4,453 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **218,192** | **277,153** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **32,552** | **29,477** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (39,981) | (39,925) |
| 34 | Faida (Hasara) ya kipindi husika | 6,912 | 3,780 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 5,097 | 5,097 |
| 36 | Stahiki ya wenyehisa chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **32,552** | **29,477** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 574,416 | 613,257 |
| 39 | Mikopo chechefu | 17,251 | 9,060 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 6,347 | 5,622 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 13% | 10% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 27% | 14% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 45% | 39% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 25% | 24% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 85% | 85% |
| (vi) | Ongezeko la amana | -26% | 10% |
| (vii) | Ongezeko la mali | -18% | 13% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-23 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-22 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya riba | 6,651 | 3,208 | 15,963 | 6,800 |
| 2 | Gharama za riba | (1,456) | (1,059) | (4,231) | (2,216) |
| **3** | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **5,195** | **2,149** | **11,732** | **4,583** |
| 4 | Madeni viza yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika Mikopo | (724) | - | (981) | - |
| **6** | **Mapato yasiyo ya riba:** | **3,346** | **3,344** | **9,894** | **6,150** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 1,792 | 507 | 4,642 | 958 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 1,534 | 2,830 | 5,178 | 5,180 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | 20 | 7 | 74 | 13 |
| **7** | **Gharama zisizo za riba:** | **(4,603)** | **(4,163)** | **(13,486)** | **(8,367)** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | (1,967) | (1,929) | (6,032) | (3,721) |
| | 7.2 Ada na kamisheni | (443) | (383) | (1,283) | (765) |
| | 7.3 Gharama nyingine | (2,193) | (1,851) | (6,171) | (3,882) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya uendeshaji** | **3,214** | **1,330** | **7,159** | **2,366** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | (82) | (137) | (247) | (250) |
| 10 | Faida / (Hasara) halisi baada ya kodi ya mapato | 3,132 | 1,193 | 6,912 | 2,116 |
| 11 | Mapato mengine yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **3,132** | **1,193** | **6,912** | **2,116** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 141 | 127 | 141 | 127 |
| 14 | Mapato kwa hisa | 498 | 190 | 1,100 | 337 |
| **15** | **Idadi ya matawi** | **8** | **7** | **8** | **7** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa faida kabla ya kodi na wastani wa mali | 4.61% | 0.67% | 5.14% | 1.18% |
| | (ii) Uwiano wa faida baada ya kodi na wastani wa fedha za wanahisa | 40.39% | 4.55% | 44.57% | 8.06% |
| | (iii) Uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 46.04% | 63.53% | 52.16% | 64.62% |
| | (iv) Uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 8.24% | 1.87% | 9.31% | 3.99% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Sep-23 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-22 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **3,132** | **2,463** | **6,912** | **1,622** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | - | - | - |
| Hasara Katika Mali | 1,136 | 752 | 1,888 | 557 |
| Badiliko Halisi Katika Mikopo | 11,094 | (12,559) | (1,465) | 2,207 |
| Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Amana | (60,672) | 34,369 | (26,302) | (2,438) |
| Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,526) | (599) | (2,125) | 9,392 |
| Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 2,276 | (201) | 2,074 | 732 |
| Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 46,335 | (27,059) | 19,276 | 11,480 |
| Kodi Iliyolipwa | (82) | (82) | (165) | (37) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | **1,693** | **(2,915)** | **95** | **23,515** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,636) | (174) | (2,810) | (4,201) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | **(2,636)** | **(174)** | **(2,810)** | **(4,201)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | - | - | - | - |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | **(943)** | **(3,090)** | **(4,033)** | **1,942** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 21,024 | 24,113 | 45,137 | 47,685 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **20,081** | **21,024** | **41,104** | **49,627** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2023** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,925) | 5,097 | - | - | 25,696 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 6,912 | - | - | - | 6,912 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | - | | - | | |
| Share issued | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(33,069)** | **5,097** | **-** | **-** | **32,552** |
| **Mwaka uliopita 2022** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (36,525) | 487 | - | - | 24,486 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,210 | - | - | - | 1,210 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | (4,610) | 4,610 | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(39,925)** | **5,097** | **-** | **-** | **25,696** |

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1. | Gbenga Makinde<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | **Imesainiwa** | 26 Oktoba 2023 |
| 2. | Benson Msangi<br>**Afisa Mkuu wa Fedha** | **Imesainiwa** | 26 Oktoba 2023 |
| 3. | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | **Imesainiwa** | 26 Oktoba 2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | Jina na Cheo Saini | Tarehe | |
|---|---|---|---|
| 1. | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | **Imesainiwa** | 26 Oktoba 2023 |
| 2. | Ebele Ogbue<br>**Mkurugenzi** | **Imesainiwa** | 26 Oktoba 2023 |

United bank of Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank of Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa, USA, Europe & UAE.

East & South Africa | Central Africa | West Africa | Europe | USA | United Arab Emirates

ubatanzania



## HABARI DODOMA

# Sheria ya uwekezaji yavutia wawekezaji kila mwezi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk.Binilith Mahenge, amesema utekelezaji wa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022 kumechochea ongezeko la wawekezaji wanaosajiliwa TIC kutoka 20 hadi 58 kila mwezi.

Dk. Mahenge alibainisha hayo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara na wawekezaji Mkoa wa Singida baada ya kuhitimisha ziara yake ya siku mbili ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani.

Alisema sheria hiyo imepunguza thamani ya mtaji unaohitajika kwa mwekezaji wa ndani kutoka Dola za Marekani 100,000 hadi 50,000 lengo likiwa ni kuvutia wawekezaji wa ndani na pia inatambua wawekezaji mahiri ambao wanapewa misamaha ya kodi inayotolewa kwenye kipengele cha wawekezaji mahiri.

Alibainisha kuwa duniani suala la uwekezaji ni ushindani kwa kila nchi kuweka mazingira ya kuwavutia wawekezaji na kuwataka wawekezaji kujisajili TIC, ili waweze kupata manufaa baada ya kutambulika.

"Ukisajiliwa TIC ukapewa na cheti tunakuwa tumekusaidia kutambulika hata ukitaka kwenda kukopa benki inakuwa rahisi kwani uwekezaji siyo wa TIC bali ni wa Watanzania wote," alisema.

Aidha, Dk.Mahenge aliziagiza halmashauri nchini kutenga maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji ili wawekezaji wanapokuja wasipate changamoto ya migogoro na kusababisha wakate tamaa ya kuwekeza.

Dk.Mahenge alisema wawekezaji wamekuwa wakipata changamoto wanapotaka kwenda kuwekeza kwenye halmashauri kutokana na kutotengwa maeneo ya uwekezaji na hata maeneo yanayotengwa wakati mwingine yanakuwa na migogoro na hivyo kuwakatisha tamaa na kuamua kwenda kuwekeza maeneo mengine.

Dk.Mahenge alisema Wilaya ya Ikungi ni mfano mzuri wa kuigwa kutokana na kutenga maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya wawekezaji wanaotaka kwenda kuwekeza katika wilaya hiyo na kuagiza wilaya zote kufanya hivyo kwani suala la uwekezaji ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi.

Alisema hivi sasa hakuna urasimu wala kucheleweshwa mwekezaji anapokwenda kutaka huduma TIC kwani kumefunguliwa dirisha moja ambapo zote zinatolewa kwa pamoja na hivyo mteja hahitaji kusumbuka kwenda ofisi nyingi kufuata huduma.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema TIC ni chombo muhimu sana kwa agenda ya maendeleo ya nchi na kwamba uwekezaji nchini unaongezeka kutokana na kuwa na rais anayezingatia masuala ya uwekezaji.

Serukamba alisema Mkoa wa Singida umejipanga kwa ajili ya uwekezaji ili kuondoa dhana iliyojengeka kwamba Singida ni ya ukame tu, lakini ukweli kuna ardhi ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji na hivi sasa uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula unaongezeka kila msimu.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Wild Flower, Grains and Oil Mill Project, Khalid Omary, alisema kiwanda hicho ambacho uwekezaji wake utakuwa zaidi ya Sh.bilioni 56 hadi kitakapokamilika kitaanza uzalishaji Desemba mwaka huu na kitatoa ajira kwa Watanzania kati ya 400 hadi 1,000 wenye ajira za kudumu na za muda.




Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Riziki Lulida (wa pili kushoto), akizungumza mbele ya Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, (wa tatu kushoto), Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini WCF, Emmanuel Humba (wa nne kushoto) na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini WCF, Rifai Mkumba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatakiwa kuelekeza fedha miradi tabianchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kutenga na kuelekeza fedha kwenye miradi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa katika sekta za nishati jadidifu, kilimo ikolojia, miundombinu na kilimo himilivu ili taifa kuwa na usalama wa chakula.

Rahma Kiriwe, mwanaharakati wa mabadiliko ya tabianchi na mazingira, alisema hayo jana jijini hapa, wakati akisoma ripoti ya uchambuzi wa fedha za miradi ya mabadiliko tabianchi ambazo zimekuwa zikiingia nchini, uliofanywa na Jukwaa la Vijana la Global Platform Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Action Aid Tanzania.

Alisema inapaswa kutenga na kuelekeza fedha katka sekta na idara zinazosimamia majanga na namna ya kukabiliana na majanga hayo kwa ustawi wa jamii na uhimilivu dhidi ya majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Pia alisema serikali ihakikishe mahitaji mahususi ya vijana katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi yanajumuishwa katika mipango na fedha zinazotengwa kwa ajili ya kukabiliana na athari kuanzia ngazi za vijiji/mitaa, wilaya hadi ngazi ya taifa.

Akizungumzia uchambuzi huo, alisema umejumuisha vijana kutoka mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Arusha, Pwani, Tanga na Kigoma, wawakilishi wa serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na TAMISEMI kwa lengo la kuchambua kwa kina ripoti ya uchambuzi wa fedha za mabadiliko ya tabianchi Tanzania.

Alisema uchambuzi umebaini kuwa Tanzania inapokea fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya kimataifa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kwa mujibu wa uchambuzi huo, asilimia 54 ya fedha zilizopokelewa zinatumika kutekeleza miradi ya kujenga uhimili dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za kilimo, misitu, uvuvi, mazingira ya bahari, mazingira na uhifadhi wa baioanuai.

Alisema matokeo haya yanawiana na vipaumbele vya serikali katika mipango na mikakati iliyopo.

Kadhalika, alisema uchambuzi umebaini kuwa serikali kupitia bajeti za kisekta inatenga fedha na kutekeleza miradi himilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Vile vile, alisema lengo la uchambuzi huo ni kufahamu upatikanaji na matumizi ya fedha za mabadiliko ya tabianchi katika sekta hizo kwasasa ili kupendekeza maboresho, kuendeleza na kuleta suluhisho kwa vikwazo ikiwemo mfumo mzima wa ufuatiliaji wa matumizi kwa njia endelevu nchini.

Mratibu wa programu za vijana wa Shirika la ActionAid Tanzania Arif Fazel, alisema ipo haja kwa serikali kuendelea kutumia vizuri fedha za mabadiliko tabianchi zinazoelekezwa kwenye kilimo ikolojia ili kuwa na usalama wa uhakika wa chakula.

# Magereza kuboresha dawati la jinsia na watoto mikoani

**Na Renatha Msungu,** SINGIDA

JESHI la Magereza nchini limeandaa mpango mkakati wa miaka mitano kwa ajili ya kuboresha dawati la jinsia na watoto katika mikoa ya kimagereza, ili watoto wapate haki zao za msingi.

Mratibu wa dawati la jinsia na watoto wa jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Daimu Mmolosha aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye ufunguzi wa dawati hilo mkoani Singida.

Mmolosha alisema kuwa dawati hilo lilianzishwa Septemba 2018 kwa kuzingatia sheria, kanuni, mwongozo, taratibu , mila na desturi zilizowekwa ili kuongeza ufanisi katika mapambano ya dhidi ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto.

Aidha, alisema jukumu la msingi la dawati hilo ni pamoja na kushughulikia masuala yote yanayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa watoto mahala pa kazi, majumbani na katika jamii inayozunguka Jeshi la Magereza.

Alifafanua kuwa lengo la kuandaa mpango mkakati huo ni kuweka muendelezo wa kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto nchini.

"Tunafanya hivi ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kupiga vita masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto,"alisema.

Akifungua dawati hilo, Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Gaudensia Mmassy alisema maandalizi ya mpango huo yamekamilika huku akilipongeza Jeshi la Magereza kwa hatua hiyo ya kupinga na kupambana na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto nchini.

Alisema mpango huo utaongeza kasi ya uelewa wa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, huku akilitaka jeshi hilo kuendeleza jitihada zake za kufungua madawati hayo katika mikoa ya kimagereza ili kuifikia jamii.

## Ukosefu 'ambulance' kwawatesa wakazi Kata ya Itale

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

WAKAZI wa Kata ya Itale katika Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, wameiomba serikali kuwasaidia upatikanaji wa gari la kubebea wagonjwa.

Ombi hilo lilitolewa na Diwani wa Kata hiyo, Fahari Mwampashi, wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Farida Mgomi uliokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi wa maeneo mbalimbali ya kata hiyo.

Alisema kata hiyo iko mbali na makao makuu ya wilaya ambako ndiko iliko Hospitali ya Wilaya na kwamba hawana usafiri wa uhakika wa kuwafikisha katika hospitali hiyo hali ambayo inahatarisha maisha ya wagonjwa.

Mkuu wa Wilaya aliitisha mkutano huo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa kampeni yake ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi kijiji kwa kijiji iliyopewa jina la 'Tunakuja kukusikiliza'.

Mwampashi alisema serikali imekamilisha ujenzi wa kituo hicho kwa Sh. milioni 500 na tayari kimeanza kutoa huduma hasa kwa kupokea wagonjwa wa nje.

Alisema tatizo kubwa huwa ni kwa kinamama wajawazito ambao inashindikana kujifungua katika kituo hicho na kutakiwa kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya ama Hospitali ya Rufani ya Mkoa ambazo ziko mbali.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Farida aliwapongeza wananchi wa kata hiyo kwa kushirikiana na serikali katika kujenga kituo hicho mpaka kikakamilika na kuanza kutoa huduma, akisisitiza kuwa kujitolea ni muhimu kwa ajili ya maendeleo yao.

Aidha, aliiagiza Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo kushughulikia suala la upatikanaji wa gari ya kubeba wagonjwa kutokana na jiografia ya kata hiyo kuwa mbali na Hospitali ya Wilaya pamoja na miundombinu ya barabara kutokuwa rafiki.

Mgomi alisema serikali ina mpango wa kugawa magari ya kubebea wagonjwa kila wilaya, hivyo Kituo cha Afya Itale nacho kitawekwa kwenye mpango huo.

Mgomi alisema: "Nimemsikia mwakilishi wenu Mwampashi akisema kina mama mpo tayari kuongeza idadi ya wananchi (kuzaa), lakini mnahofia usalama wa uzazi, ondoeni wasiwasi serikali yenu ni sikivu na hili nitasimamia mwenyewe kuhakikisha mnafurahia maisha".

# Mapya yawakuta w'biashara waliokamatwa kwa tuhuma za utoroshaji madini Chunya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya wafanyabiashara watano wa madini wilayani Chunya mkoani Mbeya kukamatwa wakitorosha dhahabu ya Sh. milioni 961, serikali imeagiza leseni zao kusimamishwa wakati taratibu za kuwafikisha mahakamani zikiendelea.

Aidha, endapo wafanyabiashara hao watathibitika mahakamani kwamba kweli walishiriki kwenye mtandao huo wa utoroshaji wa madini, leseni zao zitafutwa na hawataruhusiwa kufanya biashara hiyo mahali popote nchini.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alitoa maagizo hayo juzi wakati akizungumza na wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wilayani Chunya.

Alisema kwa sasa serikali imeweka mazingira rafiki ya kufanyia shughuli hizo na hivyo hakuna sababu ya watu kuendelea kutorosha madini.

Mavunde alisema serikali imeondoa baadhi ya tozo ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zinalalamikiwa na wafanyabiashara hao pamoja na kujenga masoko ya kuuzia madini ili kurahisisha shughuli hizo.

Alisema madini yaliyokuwa yanatoroshwa na wafanyabiashara hao yana uzito wa kilogramu 6.9 na kwamba endapo wafanyabiashara hao wangefanikiwa kutorosha, serikali ingepoteza zaidi ya Sh. milioni 68 ambazo ni ada ya ukaguzi pamoja na mrabaha.

"Kwa sasa leseni za wafanyabiashara hawa zinasimamishwa na maeneo yote wanayomiliki haitakiwi shughuli kuendelea, lakini wakishindwa kesi mahakamani tutafuta kabisa leseni zao na hawatakiwa kufanya tena biashara ya madini popote nchini," alisema Mavunde na kuongeza.

"Kuna tabia ya mtu akiharibu anatafuta leseni nyingine kwa jina lingine, niwahakikishie kwamba tutawafuata mpaka huko, katika kipindi changu sitatoa leseni kwa watu wa aina hiyo, wakatafute shughuli zingine za kufanya," alisema Mavunde.

Hivyo, aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali na vyombo vya dola kwa kutoa taarifa za watu wanaotorosha madini hayo kwa maelezo kuwa mapato yanayopatikana kutokana na rasilimali hiyo ndiyo yanatumika kuboresha huduma mbalimbali za jamii.

Awali akizungumza na wandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga aliwataja wafanyabiashara waliokamatwa kwa tuhuma hizo za kutorosha madini kuwa ni Masunga Kidishi (43), Timoth Simbu (26), Ngunje Ideshi (41), Esther John (25) na Baraka Silwani (28) wote wakazi wa Chokaa wilayani Chunya.

Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa walikamatwa Oktoba 26 mwaka huu katika Mtaa wa Kibaoni wilayani wakiwa na madini hayo aina ya dhahabu vipande 160 wakiwa hawana nyaraka wakienda kuuza nje ya mfumo wa soko la dhahabu.

Alisema wakati wanaendelea na upekuzi kwenye maeneo mbalimbali ya watuhumiwa walipata vipande 145 kwenye makazi ya mtuhumiwa Ngunje Ideshi na vingine 15 vilipatikana kwenye gari yenye namba za usajili T. 796 DTT IST iliyokuwa na watuhumiwa Timoth Simbu na Ngunje Kidishi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon alisema wataendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti utoroshaji huo wa madini ndani ya wilaya hiyo.

Alisema mbali na tatizo hilo la utoroshaji pia wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na tatizo la wizi wa kaboni zenye dhahabu kwenye maeneo mbalimbali ya wachimbaji ambalo alisema wanaendelea kulishughulikia.

Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya za mwanzo nchini kufungua masoko ya dhahabu lakini bado inakabiliwa na tatizo la utoroshaji wa rasilimali hiyo.



Wageni maalum wakinyanyua glasi juu kusherehekea maadhimisho ya miaka 280 ya Shampeni ya Moët & Chandon's yaliyoandaliwa na MMI Tanzania, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kujenga uwanja wa ndege kusafirisha mazao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imesema ipo katika mchakato wa kujenga uwanja mpya wa ndege wenye urefu wa kilomita tatu kwa ajili ya kusafirisha mazao ya kilimo na usafiri wa kawaida mkoani Njombe.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango wakati wa akifunga Maonesho ya Nne ya Viwanda vidogo katika viwanja vya Sabasaba mjini hapa.

Dk.Mpango alisema kwa kutambua fursa mbalimbali zilizopo mkoani hapa na umuhimu wa usafiri na usafirishaji serikali itajenga uwanja wa ndege ili kuwarahisisha usafiri wananchi na wafanyabiashara.

"Naomba niwajulishe wana Njombe wenzangu kwamba serikali imepanga kujenga uwanja mpya wa ndege wenye urefu wa kilometa tatu utakaowezesha ndege kubwa za abiria na mizigo," alisema Dk.Mpango.

Pia, aliwataka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kuandaa tuzo za utambuzi au mafunzo kwa wajasiriamali ambao wamethibitika kufanya vizuri.

"Leo tumemwona mzee mmoja pale ambaye anatumia teknolojia ambayo amebuni mwenyewe alirithi kutoka kwa wazazi wake," alisema Dk. Mpango.

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola, alisema "Benki ya NMB imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono na kuwezesha viwanda vidogo na wajasiriamali kupata mitaji na kuwainua katika biashara zao, kwa wastani Benki ya NMB hutoa mikopo zaidi ya 3,000 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 60 kila mwezi kwa wateja wetu wajasiriamali wadogo na kwa mwaka huu hadi kufikia septemba 2023 Benki ya NMB imeshatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo zaidi ya 26,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 400," alisema Chilongola.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema kuwa maonesho ya SIDO yamewezesha washiriki kupata mafunzo pia kuwahamasisha vijana waliotayari kuingia katika sekta ya viwanda na biashara hususani wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwapa fursa ya kujiajiri.

Mbunge wa Njombe, Deo Mwanyika na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka walimwomba makamu wa Rais kujengewa uwanja wa ndege ili kusafirisha mazao mbalimbali ikiwamo parachichi.

Msajili msaidizi kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Nassoro Mtavu akizungumza na Nipashe katika maonesho hayo alisema watu zaidi ya 100 wamepewa elimu juu ya kutofautisha kati ya majina la biashara na alama za biashara.

# Bonanza kukitangaza Kisiwa cha Pemba kufanyika Novemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHENI ya Utalii Zanzibar inatarajia kufanya bonanza la utalii, utamaduni na michezo kisiwani Pemba kwa lengo la kukitangaza na kukifufua Kisiwa cha Pemba kupitia utalii wa michezo na utamaduni.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba, alisema tamasha hilo linatarajiwa kufanyika Novemba 28 hadi Desemba 3 mwaka huu, ambalo litagharimu Sh.milioni 120.

Alisema bonanza hilo litajulikana kama 'Pemba Tour sport and Cultural Bonanza ' (PTCB), ambalo litakuwa bonanza la nne kufanyika katika Kisiwa cha Pemba, ambapo washiriki kutoka Tanzania na Afrika Mashariki.

Pia alisema Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Jumuiya ya Waongoza Misafara ya Kitalii (ZATO), inakaribisha mashirika ya ndani, kikanda na ya kimataifa kuchangia PTCB kuwa tukio la kihistoria.

Aidha, alisema bonanza hilo ni muhimu na litawaunganisha wananchi pamoja na tamaduni zao, michezo, urithi na vivutio vya asili na kusema kuwa sekta ya uatlii inachangia kwa asilimia 29.2 ya pato la taifa na asilimia 80 ya upatikanaji wa fedha za kigeni kwa Zanzibar.

Alisema kuwa katika bonanza hilo, michezo mbalimbali itachezwa ikiwamo, mchezo wa kuogelea, kuendesha baiskeli na kukimbia, mashindano ya ngalawa, kuongelea, mchezo wa ng'ombe na kuendesha baiskeli.

"Bonanza hilo, litaendelea kukitambulisha Kisiwa cha Pemba na kuwa kivutio cha utalii endelevu (utalii wa kijani), ambalo limeleta faida katika kipindi cha miaka minne kwa kuongeza wageni," alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar, Said Kassim Marine, alisema, kamisheni wameandaa bonanza hilo kwa sababu ya umuhimu wa michezo na masuala mbalimbali, miongoni mwao ni kukuza utalii wa michezo.

Alisema baraza la michezo linashirikiana na wizara husika kwa hali na mali kuona michezo iliyopotea inaibuliwa, ili kuboresha mchakato wa michezo hasa kipindi hiki cha kutimiza miaka mitatu ya uongozi Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mweka Hazina wa ZATO, Bimkubwa Omar Khamis, alisema takriban asilimia 20 ya watalii hufika Kisiwani Pemba, hivyo wataendelea kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar ili kufanikisha tamasha hilo lenye lengo la kutangaza utalii wa michezo na utamaduni kisiwani humo.

# Zanzibar mwenyeji Mkutano wa Mapitio wa Benki ya Dunia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR kwa mara ya kwanza itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa 20 wa Mapitio wa Benki ya Dunia, utakaoshirikisha wajumbe 350 kutoka nchi mbalimbali duniani.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya alisema, Tanzania ni wapokeaji mikopo na misaada kutoka Benki ya Dunia (WB).

Alisema kwa mara ya kwanza Rais wa WB, Ajay Banga, atahudhuria mkutano huo utakaofanyika kuanzia Desemba 6 hadi 8 mwaka huu visiwani hapa.

Dk. Mkuya alisema IDA hufanya mapitio kuangalia mafikio ya kutoa misaada na kubadilisha hali za watu, ambapo huangalia namna ya kubadilisha mwelekeo na kutatua changamoto zilizojitokeza katika mfumo wa mzunguko wa fedha.

Alisema Tanzania inatumia vizuri mikopo na misaada inayopatiwa hivyo WB imeamua kufanya mkutano huo kutokana na kufanya kazi zake vizuri.

Waziri huyo alitaja mafanikio yatakayopatikana kupitia mkutano huo ni pamoja na kuwakilisha nchi nyingine, kufanya tathmini ya kuwa na maendeleo ikwamo suala la miundombinu ya jamii na kuwawezesha wanawake.

Aidha, alisema katika kuwapa kipaumbele wanawake na wajasiriamali wadogo kutakuwa na maonesho maalumu ya bidhaa zinazozalishwa nchini kwa lengo la kupata fursa.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa WB Tanzania, Nathan Balete, alisema Shirika la Fedha la Kimataifa (IDA), wanaangalia zaidi kuhusiana na mapato ikiwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 zinazofanya vizuri, hivyo imekubaliwa kupatiwa msaada kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa.

Alisema kuwa kufuatia mapitio ya utekelezaji wa misaada IDA, litaipatia Tanzania zaidi ya Dola za Marekani bilioni 8.3 kwa mwaka ujao, kwamba kwa mwaka jana walitoa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 2.1.

Aidha, alisema kuwa IDA imejikita zaidi katika kusaidia mataifa mbalimbali duniani katika nchi za Afrika ili kuendeleza na kukuza uchumi.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akijumuika na wananchi pamoja wanamichezo katika mbio za kilomita 5 za Zanzibar International Marathon, zilizoanzia eneo la Ngome Kongwe jijini Zanzibar na kumalizikia Viwanja vya Bustani ya Forodhani Wilaya ya Mjini Unguja. Kushoto kwa Rais ni Mama Mariam Mwinyi na (kulia kwa Rais) Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Bara, Dk. Damas Ndumbaro. **PICHA: IKULU**

# Kipimo kubaini hatua ya awali saratani ya matiti chapatikana

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali, Hospitali ya Ampola imeleta kipimo maalumu cha kuchunguza saratani ya matiti, ambacho kina uwezo wa kugundua saratani hiyo katika hatua za awali.

Hospitali hiyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) iliandaa kambi ya siku sita iliyotoa huduma za upimaji wa saratani hiyo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Akizungumza na waandishi wa habari, Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi, Rose Malisa alisema jumla ya watu 564 waliofika katika kambi za uchunguzi.

Alisema kati ya watu hao 145 kutoka Pemba na 419 kutoka Unguja na asilimia 21 sawa na watu 120 walikutwa na uvimbe unaohitaji uchunguzi zaidi na watatu waligundulikana na saratani ya matiti. "Hospitali hii imetoa punguzo kipimo cha kupima matiti kutoka Sh.100,000 hadi Sh.30,000 kwa mwezi huu, lengo ni kuwafikia watu wote wanaohitaji huduma hii kwa urahisi," alisema Dk. Rose.

Alisema kabla ya kufanya uchunguzi walitoa elimu kwa kinamama kuwa na kawaida ya kupima saratani kwasababu hatua ya mwanzo inatibika na kuondoka kabisa.

"Kambi hizo zilifanyika kwa siku tatu Unguja na Pemba, watu watatu waligundulikana na saratani hiyo na mmoja tulimfanyia opereheni bure na wawili tuliwapeleke Hospitali ya Mnazi Mmoja," alisema Dk. Rose

Alisema jukumu la watoa afya ni kuwaelemisha watu kujichunguza wenyewe ili kujigundua iwapo watakuwa na tatizo hilo na kufika hospitali kupata matibabu.

Dk. Rose aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kupima saratani hiyo akisema haina maumivu, ndiyo sababu ya kusisitiza kinamama kujichunguza kabla haijawaathiri zaidi.

Naye Meneja Masoko wa Hospitali ya Ampola, Edson Olotu, alisema kambi hiyo ilifanyika kwasababu huu ni mwezi wa uelimishaji wa saratani ya matiti, hivyo wameungana na wenzao ili kupinga saratani katika jamii.

Alisema wanaandaa kambi ya kupima ugonjwa wa kisukari ambayo itajumuisha madaktari bingwa kutoka Cuba na Dubai kwa lengo la kusaidia matatizo ambayo hayatatuliki nchini.

Alisema: "Iwapo utagundulika na shida yeyote katika kambi hiyo basi utatibiwa kwa punguzo la fedha katika matibabu hayo ikiwa gharama Sh. milioni moja utatoa nusu yake".

# Kilichoibeba ACT kushinda uchaguzi mdogo Mtambwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA, mshikamano na wanachama kujitokeza kwa wingi kwenda kupiga kura kumetajwa kukibeba Chama cha ACT-Wazalendo kuibuka mshindi katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe uliofanyika juzi.

Imeelezwa kuwa umoja huo wa wanachama wa chama hicho uliimarisha ulinzi wa kura zao katika vituo vya kupigia kura, ikidaiwa kuwa wengi wao walibaki nje ya vituo vya kupigia kura kuhakikisha hakuna mtu mgeni anayefika kituoni huko kupiga kura.

Hata hivyo, utaratibu huo unakatazwa kisheria. Baada ya kupiga kura, mpigakura anapaswa kuondoka katika kituo cha kupigia kura.

Katika kituo cha Shule ya Uondwe Mtambwe ambako kunatajwa ni ng'ome kuu ya ACT-Wazalendo, wanachama waliweka kambi kuhakikisha hakuna mtu mgeni anayefika kwa lengo la kupiga kura.

Wakati upigaji kura ukiendelea huku kukiwa na mvua, waliodhaniwa wafuasi wa ACT waliendelea kubaki nje ya kituo hadi mwisho wa upigaji kura na kuhesabiwa matokeo licha ya kutakiwa na vyombo vya ulinzi na usalama kuondoka.

Baada ya upigaji kura kufungwa, majumuisho na utangazaji wa matokeo ulifanyika katika Shule ya Ufundi Daya Mtambwe na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, Othman Khamis Othman akamtangaza mgombea wa ACT-Wazalendo, Dk. Muhammed Ali Suleiman kuwa mshindi katika uchaguzi huo kwa kupata kura 2,449.

Katika matokeo hayo, mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hamad Khamis Hamad, alipata kura 1,531, mgombea wa Chama cha Wananchi (CUF), Said Nassor Hemed alipata kura 43 na mgombea wa Chauma, Muhammed Nassor Rashid alipata kura 22.

Kwa mujibu wa msimamizi huyo wa uchaguzi, idadi ya wapigakura katika jimbo hilo ni 6,098. Kura halali zilizopigwa ni 4,045, zilizoharibika 155 na jumla ya kura zote zilikuwa 4,200.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya matokeo hayo, mgombea wa CCM, Hamad, alisema ameridhishwa na matokeo na uchaguzi huo. Ulikuwa huru na haki.

Mwakilishi Mteule wa jimbo hilo, Dk. Suleiman alipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kuendesha uchaguzi huru na haki licha ya baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika uchaguzi huo.

Aliwashukuru wananchi wa jimbo hilo kwa kumwamini na kumchagua kuwa mwakilishi wao na kuwaahidi kuwa atahakikisha anawaleta maendeleo.

Jimbo la Mtambwe ndiko alikozaliwa na kuzikwa Maalim Seif Sharif Hamad. Ndiye mwakilishi wa kwanza wa jimbo hilo mwaka 1985 kabla ya mfumo wa vyama vingi.




Kaimu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kuhusu Kongamano la Kimataifa la Kujadili Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji na Biashara litakalofanyika mwezi ujao mkoani Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Benki yaja na utaratibu wa kusaidia gharama za mazishi

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kuwezesha wananchi kutimiza ndoto zao na kujenga taifa, Benki ya Stanbic Tanzania imezindua huduma mpya ikilenga kusaidia watu wenye mshahara kutimiza ndoto zao na kuinua uchumi wa taifa.

Huduma hiyo inajumuisha usalama wa kifedha; mmiliki wa akaunti ya iliyoipa jina la 'Wezesha', atapatiwa fedha za kusaidia mazishi ikiwa atafariki dunia mwenyewe, mke au mtoto, hivyo kumfanya mtu awe na utulivu katika kipindi kigumu cha msiba.

Wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo mwishoni mwa wiki, uliohudhuriwa na maofisa rasilimali watu jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa benki hiyo, Omar Mtiga, alisema huduma ya Wezesha inathibitisha nia ya Stanbic kuwawezesha Watanzania kufikia malengo yao binafsi na ya taifa.

Alisema kuwa kupitia huduma hiyo, mmiliki wa akaunti hiyo atapata huduma zaidi ya zile za kifedha ikiwamo fursa za uwekezaji, elimu ya fedha na mkopo wa bima.

"Huduma ya Wezesha inawalenga watu wenye mshahara na imesanifiwa maalum kwa ajili ya kuhakikisha ndoto zao zinatimia," alisema.

Vilevile, alisema huduma hiyo inamwezesha mwajiriwa kulipia bima ya afya na biashara na hivyo kumpa urahisi wa kupata huduma hizo.

"Mwenye akaunti ya Wezesha anaweza kutoa hadi Sh. milioni 20 dirishani bure, kuhamisha fedha bure na kulipia huduma za serikali, hivyo kumpa uhuru wa kifedha.

Pia alisema kuwa mwenye akaunti atapata huduma kama vile mkopo wa bima na huduma za bure za uwekezaji.

Alisema Benki ya Stanbic inatambua umuhimu wa mafanikio binafsi, ustawi wa familia na malengo ya Watanzania kuishi mtindo wa maisha wanaoutaka.

# Mkenda azindua ufadhili wa masomo wanafunzi wa kike

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amezindua Programu ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ya Ubora kwa Ufadhili wa Masomo (TES) ambayo inakusudia kuongeza udahili kwa wanafunzi wa kike katika maeneo maalum ya kipaumbele hususani mafunzo ya anga.

Kabla ya kuzindua mpango huo katika kampasi kuu ya chuo iliyoko Mabibo, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Prof. Mkenda aliwapongeza kwa kuanzisha mpango huo wa ufadhili wa masomo. Wanafunzi wengi wa kike watanufaika na programu hiyo wakiwamo wanaotoka vijijini.

Waziri pia alipongeza NIT kwa kunufaika na Mradi wa Ujuzi wa Mageuzi na Utangamano wa Kikanda wa Afrika Mashariki (EASTRIP) ambao uko chini ya Benki ya Dunia. Unafadhili masomo kwa wasichana 11 wanaosomea mafunzo ya anga.

"Ninawapongeza kwa kupata mradi huu wa ESTRIP wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 21.25 (zaidi ya Sh. bilioni 49b) kama msaada wa kifedha kutoka Benki ya Dunia, kiwango mlichopata NIT ni zaidi ya kile ambacho wanufaika wengine kutoka Tanzania walipata; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo cha Ufundi Arusha," alisema.

Waziri Mkenda aliitaka NIT kuendelea kuzalisha rasilimali watu ya kutosha kwa lengo la kukidhi mahitaji makubwa ya usafiri na usafirishaji. Kuna mahitaji makubwa ya wafanyakazi katika sekta hiyo.

"Serikali inajivunia sana kuona NIT wanaweza kwa kiasi kikubwa kusimamia matumizi ya fedha na sisi kama serikali tutaendelea kufanya kila tuwezalo kukidhi mahitaji yao na nina uhakika kwamba NIT itaendelea kuwa chuo bora," alisema.

Prof. Mkenda alisema lengo la serikali ni kuona wanafunzi wengi wa Kitanzania wanapata vyeti vya kimataifa na kuwa na uwezo wa kufanya kazi nje ya nchi.

"Mbali na wanafunzi wanaosomea shahada ya kwanza, serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa sasa imeamua kuwapa nafasi wanafunzi wanaosomea stashahada kupata mikopo. Na kozi nyingi ambazo zimechaguliwa, zipo NIT," alisema.

Akiwa NIT, Prof. Mkenda pia aliweka mawe ya msingi katika majengo yanayoendelea kujengwa na CRJE; majengo mawili ya hosteli za wanaume na majengo mengine yanajengwa na NANDHRA Engineering Construction Company Ltd ambayo ni pamoja na Kituo cha Majengo ya Ubora (ghorofa tatu); jengo la Hi-Tech na Jengo la Maabara (ghorofa mbili), jengo la Mock-up na jengo lingine la ghorofa mbili.

Ujenzi wa majengo hayo ni sehemu ya msaada kutoka kwa mradi wa Benki ya Dunia wa EASTRIP ambao unawaandaa wataalamu kufanya utafiti na ushauri kwa maendeleo ya taifa.

Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa alisema: "Maono yetu ni kuona chuo chetu kinakuwa kituo cha ubora cha kikanda katika usafirishaji, usimamizi na teknolojia ya usafirishaji ya kutoa elimu inayokubalika katika usafirishaji na endelevu."

Prof. Mganilwa pia alisema taasisi yao imeanzisha vituo viwili vya ubora katika usafirishaji kwa uchumi endelevu kikiwamo Kituo cha Umahiri katika Uendeshaji wa Usafiri wa Anga na Usafiri (CoEATO) kilichoanzishwa kupitia mradi wa EASTRIP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na pamoja na Kituo cha Umahiri katika Usalama Barabarani kilichoanzishwa kupitia mradi wa ujenzi wa barabara chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

HABARI KITAIFA/KIMATAIFA

# Iran yatoa angalizo kwa Israel

**TEL AVIV,** Israel

RAIS wa Iran, Ebrahim Raisi, ametoa angalizo kuwa hatua za Israel zimevuka mipaka na zinaweza kulazimisha kila mtu kuchukua hatua kutokana na kinachoendelea katika ukanda wa Gaza, Palestina.

Akiandika kwenye mtandao wake wa X (zamani Twitter) jana Rais Ebrahim, alionyesha kushangazwa akisema "Washington inatutaka tusifanye lolote, lakini wanaendelea kutoa uungaji mkono mkubwa kwa Israel".

Inaelezwa kuwa Marekani ilituma ujumbe kwa mhimili wa upinzani lakini ilipata jibu la wazi kwenye uwanja wa vita kwamba mhimili huo unarejelea mtandao wa vikosi vinavyoungwa mkono na Iran kote mashariki ya kati, ambayo Hamas ni sehemu yake.

Mamlaka za Marekani zimekuwa zikiionya Iran kujiepusha na vita vya Israel na Hamas kwani wana nia ya kusitisha mzozo huo, licha ya kundi la Hezbollah lenye makazi yake nchini Lebanon na kuungwa mkono na Iran, limekuwa likipambana na Israel katika wiki za hivi karibuni.

Aidha, wakati hayo yakiendelea Jeshi la Israel liliweka picha kwenye mtandao wake wa X zinazoonyesha wanajeshi wake wakijiandaa kwa shughuli za ardhini huko Gaza.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema Israel imeingia katika hatua ya pili ya vita vyake na Hamas, na imeweka wanajeshi na makamanda kote katika Ukanda wa Gaza.

Alieleza kwamba hiyo itakuwa vita ndefu na ngumu, kwamba watapigana hawatasalimu amri na watashinda, huku akisisitiza kuwa hawata jiondoa.

### WAPORA MISAADA

Kwa upande mwingine Shirika la Umoja wa Mataifa la Kazi na Misaada kwa Wakimbizi wa Palestina (UNRWA) limebainisha kuwa maelfu ya watu wamevunja maghala na vituo vya usambazaji wa misaada katika eneo la kati na kusini mwa Ukanda wa Gaza, na kuchukua vyakula na bidhaa nyingine muhimu.

Mkurugenzi wa UNRWA, Thomas White, alisema ishara hiyo inatia wasiwasi kwamba utaratibu wa kawaida wa kiraia utavurugwa baada ya wiki tatu za vita na mzingiro kwa Gaza, akieleza kuwa watu wanahofu, wamechanganyikiwa na pia wamekata tamaa.

Ilielezwa kuwa hali ya usambazaji bidhaa Gaza ilikuwa mbaya hata kabla ya vita kuanza na imezidi kuvurugika kutokana na mzingiro na kusambaratika kwa watu.

Takriban malori 80 yenye bidhaa yaliingia katika Ukanda wa Gaza kutoka Misri kupitia kivuko cha mpaka cha Rafah tangu vita vilipozuka wiki tatu zilizopita. Na kwamba tangu Jumamosi hakuna msafara ulioweza kuingia Gaza kutokana na kuharibika kwa miundombinu ya mawasiliano kwasababu ya mashambulizi yanayoendelea.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa mawasiliano ya simu na intaneti katika mji wa Gaza, yaliyoharibiwa vibaya Ijumaa usiku wakati ndege za Israel zilipodondosha mabomu na askari wake kuingia katika eneo hilo linalotawaliwa na Hamas.

Ilielezwa kuwa kuvurugwa kwa mawasiliano kuliathiri operesheni za uokozi, huku watu waliokumbwa na mashambulizi ya angani wakishindwa kuomba msaada.

Kanali Goren wa Cogat, Shirika la Wizara ya Ulinzi ya Israel linaloratibu na Wapalestina, alisema Israel itaruhusu ongezeko la misaada Gaza katika siku chache zijazo na raia wa Kipalestina wanapaswa kwenda wanapopaita eneo la kibinadamu kusini mwa Ukanda huo mdogo. **BBC, DW**

## Waridhishwa huduma WCF

**Na Mwandishi Wetu**

WAJUMBE wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, wameridhishwa na huduma zitolewazo na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) baada ya kusikiliza ushuhuda wa baadhi ya wanufaika wa fidia, kamati hiyo ilipotembelea ofisi za mfuko huo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Riziki Lulida, wajumbe hao walipata fursa ya kupata maelezo ya utekelezaji wa shughuli za mfuko kutoka kwa watendaji wa mfuko kabla ya kusikiliza ushuhuda.

"Niwapongeze WCF kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya, nitapeleka salamu kwa Rais ambaye amekuwa mstari wa mbele kusaidia makundi mbalimbali yakiwamo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Na hili mnalofanya, mnamfanya ajivunie huduma mnazotoa kwa wananchi," alisema Riziki.

Katani Katani, mjumbe wa kamati hiyo, alipongeza huduma za WCF ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa faraja kwa wafanyakazi wanaoumia, kuugua ama kufariki dunia kutokana na kazi.

Wajumbe hao pia walishauri kufanyike marekebisho ya sheria kuhusu ukomo wa kuwasilisha madai kwa mtu anayeumia kutokana na ajali. Sheria iliyopo imeweka ukomo wa miezi 12.

"Jambo hili ningeshauri lifanyiwe marekebisho, ili kwa mtu aliyechelewa kuwasilisha taarifa kutokana na sababu mbalimbali, aweze kuruhusiwa kuwasilisha madai na hapa atakuwa amepata haki yake," alishauri Michael Kembeki.

Ester John, mnufaika wa fidia kama mtegemezi, mumewe ambaye alikuwa mtumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, alifariki dunia katika ajali ya gari wakati akitekeleza majukumu ya mwajiri wake.

"Wakati tunampoteza mpendwa wetu, mimi nilikuwa ugenini, sina ndugu yeyote. Nilifanyiwa operesheni ya uzazi, WCF ilitusaidia, mafao ya kila mwezi ninayoyapokea yanasaidia kuendesha maisha yangu pamoja na mtoto," alisema.

Mnufaika mwingine, Hassan Jambau, aliwaambia wajumbe hao kuwa tangu alipoumia hadi kupona na kubaki na ulemavu wa mguu, WCF imekuwa pamoja naye.

Kelvin Mwemezi, ambaye naye aliumia mguu baada ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali, alisema mfuko umekuwa msaada mkubwa na umekuwa kama sehemu ya familia yake baada ya kupoteza wazazi wake.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemabvu), Patrobas Katambi, aliwashukuru wajumbe wa kamati hiyo kwa kutembelea WCF ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Cyprian Luhemeja, alisema kuwa kwa niaba ya serikali, wamepokea ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na wajumbe ili kuhakikisha kazi nzuri inayofanywa na mfuko inakuwa bora zaidi.

"Tutajaribu kuangalia yale yanayowezekana kubadilishwa kisera tutayarekebisha na yale yanayohusiana na taratibu za ILO (Shirika la Kazi la Kimataifa) nayo tutajaribu kuangalia namna nzuri ya kutekeleza majukumu yetu," alisema Luhemeja.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma alisema WCF imeendelea kujenga mifumo ya kufanyia kazi ili kurahisisha upatikanaji huduma kwa wanachama.



Kikosi cha wanajeshi wa Israel kikitembea na vifaru katika eneo moja wapo ndani ya ukanda wa Gaza, jana. **PICHA: MTANDAO**

# MAJIHA ATOA ZAWADI KWA RAIS SAMIA UBINGWA WBC

**Na Saada Akida**

BONDIA Fadhili Majiha, amefanikiwa kushinda mkanda wa Ubingwa wa WBC Afrika kwa kumchapa kwa pointi mpinzani wake, Bongani Mahlangu wa Afrika Kusini huku akitoa zawadi ya ubingwa huo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.

**Majiha au 'Kiepe Nyani' alishinda pambano hilo kwa ushindi wa majaji wote watatu katika pambano hilo lililopigwa juzi kwenye Ukumbi wa PTA Sabasaba chini ya Kampuni ya Promosheni ya Ngumi za Kulipwa nchini, HB SADC Boxing.**

Katika pambano hilo ambalo lilipigwa kwa raundi kumi, Majiha alifanikiwa kuonesha mchezo mzuri kutokana na kutawala katika raundi zote huku akimpeleka chini Bongani katika pambano hilo kabla ya kutangazwa mshindi.

Mtanzania huyo ameshinda ubingwa huo ikiwa ni mara ya kwanza kwa Afrika kupiganiwa tangu kuzinduliwa kwa mkanda huo huku pambano likisimamiwa na Makamu wa Rais wa Baraza la Ngumi Duniani (WBC), Houcine Houichi.

Baada ya pambano hilo, Majiha alisema anamshukuru Mungu na Watanzania kwa kuweza kumwombea kushinda pambano hilo huku akiutoa ubingwa huo zawadi kwa Rais Samia.

"Nashukuru Mungu kwa kuweza kunisaidia, kushinda pambano bila ya kusahau dua za Watanzania ambao wameniombea kushinda ubingwa huu wa WBC Afrika ambao Majiha ndiyo bingwa wake wa kwanza.

"Ubingwa wa kwanza wa WBC Afrika, umechezwa Tanzania na nimeweza kumpiga vizuri Bongani kila mmoja ameona, basi nichukue nafasi hii kutoa zawadi ya huu ubingwa kwa Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi anazozifanya kutulea sisi," alisema Majiha.

Kwa upande wa Bongani, alilalamikia kitendo cha pambano hilo kuchezwa kwa raundi kumi badala ya 12 hali iliyosababisha kuomba pambano la marudiano litakalopigwa kwa raundi 12 ili kuweza kumaliza utata.

Naye Ibrahim Class amefanikiwa kutetea mkanda wake wa ubingwa wa Taifa wa TPBRC kwa kumchakaza mpinzani wake, Xiao Tau Su kutoka China katika pambano ambalo limepigwa kwa raundi kumi.

Mbali ya Ibrahim Class, Stumai Muki naye alifanikiwa kuibuka na ushindi wa pointi dhidi ya Himanshi Bhondsi wa India katika pambano la raundi nane wakati Egine Kayange akimchapa Maimuna Hashim kwa TKO ya raundi ya pili katika pambano la raundi sita.

John Chuwa aliibuka na ushindi wa pointi dhidi ya Richard Mkude katika pambano la raundi sita wakati Leyla Macho akifanikiwa kumchakaza kwa pointi Fatuma Juma huku Luqman Ramadhani akimchapa Anthony Mathias wakati Shomari Milundi akimbomoa kwa pointi Nurdin Makame.



Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Yanga, Ally Kamwe (kushoto) akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano NIC Insurance, Karim Meshack, wakazingumza na waandishi wa habari wakati wakitangaza tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwezi inayodhaminiwa na NIC Insurance mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Shirika hilo la bima lenye tunzo ya Superbrand Ukanda wa Afrika ya Mashariki, linakabidhi kitita cha Sh. milioni nne kwa mchezaji bora kwa kuzingatia vigezo tofauti ikiwamo mchango wake katika kuisaidia timu kufanya vizuri kwenye michezo tofauti ndani ya mwezi, ikiwa ni udhamini utakaodumu kwa misimu mitatu kuanzia mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kocha Mafunzo ataja majeruhi sababu vichapo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Maafande wa Mafunzo SC, wakiendelea kupokea matokeo mabaya katika Ligi kuu ya Zanzibar baada ya juzi kuchezea tena kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga SC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdallah Bakari 'Edo', analia na wimbi la majeruhi katika kikosi chake.

Katika mchezo huo uliochezwa katika Uwanja wa Mau majira ya saa 10 alasiri, mabao ya Kipanga yalifungwa na wachezaji Kabasele Hamadi dakika ya 82 na Ahmad Abdulla dakika ya 90.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Edo, amesema tatizo kubwa linaloikumba timu hiyo kwa sasa ni kuwa na majeruhi wengi katika kikosi chake.

Alisema mpaka sasa anajumla ya wachezaji majeruhi 11 ambao kati ya hao wachezaji sita ni kutoka kikosi cha kwanza.

Alisema kila timu inaposhuka dimbani lazima wapatikane wachezaji majeruhi ambao wanawafanya kushindwa kucheza mchezo ulipo mbele yao.

Alisema kama mwalimu alichukua jitihada kadhaa ikiwamo kuwapandisha wachezaji watano kutoka timu ndogo ili kuisaidia timu hiyo jambo ambalo haikuwa mipango ya timu hiyo.

"Majeruhi ndio wanaonitesa kwa sasa, tulifanya mazoezi vizuri na tulijiandaa na msimu kwa kucheza michezo mingi ya kirafiki, lakini baada ya michezo mitatu naambulia kupata majeruhi kila tukishuka uwanjani, tena majeraha ambayo mchezaji anatakiwa apate mapumziko ya muda mrefu," alisema.

Aidha, alisema katika uchunguzi wake amebaini baadhi ya wachezaji katika kipindi cha mapumziko ya msimu hutumia muda wao vibaya kwa kucheza mashindano ya mitaani.

Alisema hali hiyo inasababisha viungo vya mwili kuchoka kwa sababu ya kupumzika kwa muda mfupi wanapoanza maandalizi ya msimu.

Hata hivyo, kocha huyo alisema kwa sasa anaelekeza nguvu zake kwa wachezaji wa timu ndogo ambao amewapandisha kucheza timu kubwa ili waweze kucheza vizuri mpaka dirisha dogo litakapofunguliwa ili kuzipa mapengo yaliopo.

Klabu ya Mafunzo katika michezo nane iliyocheza hadi sasa imeshinda mchezo mmoja, sare tatu na kupoteza minne, hivyo kushika nafasi ya 12 na alama zake sita katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar

## Namungo na moto Azam FC kwa Coastal

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Klabu ya Namungo, limesema kwa sasa linaelekeza nguvu zake kwenye mchezo ujao dhidi ya Coastal Union utakaopigwa keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Denis Kitambi, alisema ushindani waliouonesha kwenye mchezo uliopita dhidi ya Azam FC watauendeleza dhidi ya Coastal Union.

"Ninaamini kikosi changu kutokana na maandalizi ninayoyafanya matokeo yaliyopita yamewapa nguvu wachezaji wangu ya kufanya vizuri katika mchezo huo," alisema Kitambi.

Alisema makosa madogo madogo anaendelea kuyafanyia kazi ili yasijirudie kwenye mchezo huo.

Aliwataka mashabiki wao wasikatishwe tamaa na nafasi waliyopo kwani bado wana nafasi ya kufanya vizuri.

"Ninaomba mashabiki wangu waendelee kutuunga mkono kwani malengo yetu ni kuendelea kusalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema.

## KenGold haikamatiki Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Kengold imezidi kujichimbia kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship baada ya kutoa kichapo cha mabao 2-0 dhidi Biashara United.

KenGold, timu yenye maskani yake Mbeya, ilishuka kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera na kutoa kipigo hicho kilichozidi kuiweka juu ya msimamo wa ligi hiyo ikiwa imefikisha jumla ya pointi 19 kwa mechi nane ilizocheza.

Timu hiyo imeshinda mechi sita, sare moja na ikipoteza mechi moja tu. Mbali na mechi hiyo, timu ya Pan African ilijitutumua na kupata ushindi wake wa pili msimu huu kwa kuifunga FGA Talents mabao 2-1, mechi ikipigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ruvu Shooting bado imeendelea kuwa kibonde kwenye ligi hiyo ikidunguliwa bao 1-0 dhidi ya Copco kwenye uwanja wake inaotumia kama wa nyumbani kwa sasa, Jamhuri Dodoma.

Timu hiyo inaendelea kuburuza mkia ikiwa imecheza mechi nane, ikipoteza sana na kutoa sare moja, huku dalili zikionesha kuwa huenda inaweza kushuka hadi Daraja la Pili 'First League' kama hatua madhubuti ya kuinusuru hazitachukuliwa.

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS PAUNI MILIONI 50

MANCHESTER City imeweka dau la pauni milioni 50 kwa kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, na wamedhamiria kupata faida kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, baada ya kuilipa Leeds United pauni milioni 42 mwaka jana. ***(Mirror)***

### DE BRUYNE MSHAHARA JUU

KLABU za Saudi Arabia zinapanga kumpa kiungo wa kati wa Manchester City na Ubelgiji, Kevin De Bruyne mwenye umri wa miaka 32, kitita kikubwa cha mshahara mwaka 2024. ***(Football Insider)***

### AMTAKA TCHOUAMENI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anamtaka kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 24, huku mchezaji wa Kimataifa wa Real Madrid na Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye miaka 23, pia akiwavutia. ***(Mirror)***

### MARQUINHOS AWINDWA

KLABU ya Arsenal itafikiria kumweka winga wa Brazil, Marquinhos mwenye umri wa miaka 20, kwenye mipango yake ya uhamisho wa Januari. ***(Mail)***

### OSIMHEN HAONDOKI NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24, amepuuza mapendekezo kwamba ana nia ya kuondoka Napoli huku kukiwa na ripoti ya kutakiwa Liverpool. ***(Mirror)***

### NEVES KUTUA NEWCASTLE

KIUNGO wa kati wa Al-Hilal, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 26, "ana ndoto" za kupata uhamisho wa Januari kwenda Newcastle United, ambayo itamlenga mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno baada ya kuthibitishwa kufungiwa kwa Sandro Tonali kwa miezi 10. ***(O Jogo via Sporting witness)***

### NEWCASTLE YASAKA NYOTA

KLABU ya Newcastle United itaziba nafasi ya Sandro Tonali kwa kumsajili kwa mkopo mchezaji wa Kimataifa wa Ureno na Fulham mwenye umri wa miaka 28, Joao Palhinha. Pia inawataka Amadou Onana wa Everton mwenye miaka 22, na kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay mwenye miaka 26. ***(Football Insider)***

### CITY YAMMULIKA MUSIALA

MANCHESTER City na Liverpool zinafuatilia hali ya mshambuliaji wa Bayern Munich, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20, ambaye atashinikiza kuhama Januari ikiwa hatapata muda wa kutosha wa kucheza. ***(Football Insider)***


### NETO NA ARSENAL

MPANGO wa Arsenal wa uhamisho wa Januari unaweza kutegemea ukubwa wa jeraha alilopata mshambuliaji wa Wolves na Ureno, Pedro Neto, katika mchezo wa timu yake dhidi ya Newcastle Unite Jumamosi. ***(Mail)***

### EMERY AIPAGAWISHA CITY

MANCHESTER City pia bado wanavutiwa na kiungo wa kati wa Paris Saint-Germain, Mfaransa Warren Zaire-Emery, 17. ***(Sport Zone, TeamTalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: NILIJUA NKETIAH ATAIBEBA ARSENAL EPL

**LONDON,** England

Ni baada ya kupiga hat-trick, asema ana jicho la goli, angalia takwimu za miaka...

MIKEL Arteta alimsifu Eddie Nketiah kwa "kiwango cha juu" baada ya mshambuliaji huyo wa England kupiga hat-trick yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu England katika ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya klabu iliyo mkiani mwa msimamo, Sheffield United, Jumamosi.

**Ushindi huo uliwapeleka 'Washikabunduki' hao hadi nafasi ya pili - pointi mbili nyuma ya viongozi na wapinzani wao wa London Kaskazini, Tottenham Hotspur huku vijana wa Arteta wakiwa hawajapoteza baada ya mechi 10 za ligi.**

Huku Gabriel Jesus akikabiliwa na tatizo la msuli wa paja kwa wiki chache, Nketiah - ambaye alitoa hat-trick hiyo kwa marehemu shangazi yake kwa mara nyingine tena, alipewa jukumu la kuwa mshambuliaji wa kati.

Alifunga mara tatu na kumaliza mchezo akiwa na kitambaa cha unahodha huku Takehiro Tomiyasu na Fabio Vieira pia wakifua moja moja katika ushindi huo mnono.

Arteta alisema: "Kwangu mimi ni wa kiwango cha juu.

"Ameanza michezo nane kati ya 10 ya Ligi Kuu. Kwa hiyo inakuambia jinsi tunavyomwamini, jinsi ninavyomwamini na umuhimu alionao katika timu.

"Nina furaha sana kwake, mchezaji wa akademi kupata hat-trick kwenye Ligi Kuu.

"Anahitaji kufurahia wakati huu. Anastahili kabisa na tunatumaini kuna wengine wengi zaidi.

"Ana jicho la goli. Unaangalia takwimu za miaka yake 10 iliyopita.

"Alichofanya ni cha kushangaza na anahitaji dakika, fursa na huduma na ikiwa atapata hiyo, Eddie atafunga mabao, hiyo ni hakika."

# ANCELOTTI: NASHANGAZWA KIWANGO CHA BELLINGHAM




**BARCELONA,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema "ameshangazwa" na jinsi Jude Bellingham anavyoendelea kupachika mabao baada ya kiungo huyo wa kati wa Real Madrid kufunga mabao mawili katika ushindi wa 2-1 wa El Clasico dhidi ya Barcelona Jumamosi, akisema kwamba "hivi sasa yeye ndiye mchezaji anayeleta mabadiliko."

Bellingham aliisawazishia Real Madrid dakika ya 68 kwenye Uwanja wa Olympic baada ya Ilkay Gündogan kuiweka Barca mbele dakika ya sita - kabla ya kufunga bao la ushindi katika muda ulioongezwa na kuwaacha Madrid kileleni mwa msimamo wa LaLiga kwa pointi 28.

"Alifunga bao la ajabu la kwanza na alikuwa mwerevu kwa la pili," alisema Ancelotti katika mkutano wake na wanahabari baada ya mechi.

"Tunashangaa. Kila mtu anashangazwa na kiwango chake, na kiwango chake cha ufanisi pale mbele.

"Anaingia kwenye eneo la hatari, lakini leo (juzi) shuti la bao la kwanza lilitushangaza, alifunga bao zuri sana... Hivi sasa yeye ndiye mchezaji anayeleta mabadiliko."

Nyota huyo wa England sasa ana mabao 10 katika mechi 10 za ligi msimu huu na kumfanya kuwa mfungaji bora kwa sasa na 13 katika mashindano yote baada ya kufunga matatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Anaonekana kama mkongwe, mtazamo wake ni mzuri sana," Ancelotti alisema. "Bao la kusawazisha lilibadilisha nguvu kabisa, lilimaanisha nguvu zaidi kwetu na udhaifu zaidi kwa Barcelona, ambao walikuwa wamecheza vema hadi wakati huo."

Mshirika wa Bellingham katika nafasi ya kiungo, Luka Modric aliongeza sifa kwake.

## Wazazi wa Diaz watekwa, mama aokolewa

**BOGOTA,** Colombia

RAIS wa Colombia, Gustavo Petro, amesema kwamba mama mzazi wa mchezaji wa Colombia na Liverpool, Luis Diaz, aliokolewa Jumamosi baada ya kutekwa nyara kaskazini mwa nchi hiyo, lakini maofisa wanaendelea kumtafuta baba yake aliyetoweka.

Ofisi ya mwanasheria mkuu wa Colombia hapo awali ilisema ilikusanya timu ya wachunguzi kuwatafuta wanandoa hao huko Barrancas, manispaa ya jimbo la kaskazini mwa Colombia la La Guajira.

Polisi walithibitisha kuokolewa kwa mamaye Diaz, Cilenis Marulanda, na kusema alizungumza na Mkurugenzi William Rene Salamanca. Katika video, Salamanca alisema anatumia kila namna kumtafuta baba yake Diaz.

Wazazi wa Diaz mwenye umri wa miaka 26, waliripotiwa kutekwa nyara walipokuwa wakiendesha gari kuelekea nyumbani kwao. Watu wenye silaha waliokuwa kwenye pikipiki waliwasimamisha na kuwashusha kwenye gari, mamlaka ilisema.

Shirikisho la Soka nchini Colombia lilisema katika taarifa yake kwamba utekaji nyara huo ni wa kusikitisha na kuwataka viongozi kumwokoa baba huyo.






## *Kane alifurahishwa na bao la ajabu*

**MUNICH,** Ujerumani

HARRY Kane alikiri goli lake la pili lilikuwa la ustadi alilofunga katika kipindi chake cha uchezaji kwenye ushindi wa mabao 8-0 wa Bayern Munich dhidi ya Darmstadt na lilikuwa mojawapo ya mabao yake bora kuwahi kutokea.

Mshambuliaji huyo wa England alimwona mlinda mlango nje ya safu yake na akapiga shuti zuri la juu na kujaa wavuni hali iliyosababisha kulinganishwa na wachezaji wenzake wa zamani wa England, David Beckham na Wayne Rooney.

Lilikuwa bao la pili katika hat-trick ya Kane, kwenye mchezo huo Jumamosi, ambaye aliingia kwenye mitandao ya kijamii baada ya mchezo huo.

Alisema: "Ni wazi lilikuwa moja ya mabao bora ambayo nimefunga katika maisha yangu hadi sasa.

"Nilipata mpira kwenye nusu ya uwanja na nilimwona kipa akitoka nje ya mstari wake katika kipindi chote cha kwanza.

"Siku zote ninatafuta kila mchezo na bila shaka nimejaribu kufunga kutoka katikati ya mstari mara chache katika kazi yangu, lakini hii ilitoka kikamilifu.

"Mchana maalum, haswa kumaliza kwa hat-trick pia. Kwa hivyo ndio, tunaendelea kwa wiki ijayo."

Kane alifunga hat-trick yake ya pili msimu huu kwenye Bundesliga huku Bayern ya wachezaji 10 ikirejea kutoka bila goli dakika 45 za kwanza na kuwashinda wachezaji tisa wa Darmstadt 8-0 kwenye uwanja wa Allianz Arena.

Joshua Kimmich wa Bayern alitolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya dakika nne pekee, lakini kadi nyekundu za Klaus Gjasula na Matej Maglica ziliwafanya Darmstadt kumaliza na wachezaji tisa.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa wachezaji watatu kutolewa nje kwa kadi nyekundu katika kipindi cha kwanza cha mechi ya Ligi Kuu ya Ujerumani.

## Baleke, Aziz Ki

INATOKA UKURASA 24

alikuwa uwanjani kuitazama Simba ikicheza dhidi ya Ihefu SC na tayari ameanza kuandaa dawa ya kuhakikisha anapata ushindi Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Gamondi alikuwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, akiliongoza jopo la benchi lake la ufundi, wakiwamo watu wa kutathmini na kuchambua mechi za wapinzani kwa ajili ya kuiangalia Simba ambayo watacheza nayo Jumapili wiki hii.

Kocha huyo pamoja na watu wake waliokuwa kuwa makini sana, mmoja akiandika baadhi ya vitu alivyoona vinafaa kufanyiwa kazi, huku Gamondi mara kwa mara akiwauliza maswali.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kwa sasa wameanza kujiandaa na mechi dhidi ya watani zao Simba, huku msingi mkubwa ukiwa kwa wachezaji watatu, Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli na Pacome Zouzoua ambao wanaamini ndiyo watakaomaliza mechi hiyo.

"Tunamshukuru kocha wetu Gamondi, yeye ndiyo kiongozi wa plani zote, kuangalia timu pinzani na kuandaa mikakati, kwa sasa anawaandaa wachezaji baada ya kile alichokiona na kila kitu kitaonekana kwa Mpaka Novemba 5.

"Tuna Aziz Ki, Nzengeli na Pacome, wote kwanza kabisa ni mawinga kiasili, lakini wanaweza kucheza kwa uhakika kabisa namba 10, halafu ukienda mbali zaidi wana sifa zinazotofautiana, mwingine anaweza kukaa na mpira muda mrefu, mmoja anaweza kukokota na kukimbia nao, mwingine ana uwezo mkubwa wa kupiga mashuti, hawa wote wanaandaliwa kwa kazi hiyo tu," alisema Kamwe.

Kamwe alisema kuwa kama walivyokuwa wakiomba, walitaka kwenda kwenye dabi huku wakiwa kileleni na ndivyo ilivyotokea.

"Tulikuwa tunataka kucheza mechi ya dabi tukiwa kileleni ili tukifungwa tushushwe na siyo kwenda kugombea kushinda ili tupande juu na ndivyo ilivyo sasa, tupo juu ya msimamo wakitaka watufunge ili watushushe, alisema Kamwe.

# MO AWAPA RUNGU SIMBA RAGE, KABURU, AVEVA NA KADUGUDA

**Na Adam Fungamwangwo**

RAIS wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, ameteua wanachama 21 wa klabu hiyo kuwa wajumbe wa Bodi ya Baraza la Ushauri wa klabu, ambapo baadhi walioteuliwa ni watu maarufu waliowahi kuwa viongozi wa nyadhifa mbalimbali, akiwamo Ismail Aden Rage, Geofrey Nyange 'Kaburu', Hassan Dalali, Azim Dewji, Kassim Dewji, Swedi Nkwabi, Evance Aveva, Mwina Kaduguda na wengineo.

**Katika uteuzi huo alioutangaza jana mchana, Mo amesema mojawapo ya majukumu yake kama Rais wa Heshima ni kuhakikisha uongozi na utawala bora unazidi kuboreka kila wakati ili kuzidi kusukuma gurudumu la maendeleo ya klabu hiyo.**

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tangu tuanze safari ya mabadililko klabu yetu imepiga hatua kubwa sana katika nyanja mbalimbali.

Pamoja na maendeleo ambayo klabu yetu imepiga katika kipindi hiki cha miaka mitano, lakini malengo yetu bado hatujayafikia.

Hivyo basi, baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi na Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, nimewateua wanachama hawa kuwa Wajumbe wa Baraza la Ushauri (Advisory Board) la Klabu ya Simba," alisema Mwekezaji huyo.

Jaji Thomas Mihayo ndiye aliyechaguliwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, huku wajumbe wake wengi wakiwa waliowahi kushika nyadhifa kwenye klabu hiyo kama Uenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Rais wa Klabu, Katibu Mkuu, Mfadhili Mkuu na nyinginezo.

Mbali na hao, wengine walioteuliwa ni Faroukh Baghoza, Musleh Al-Ruweh, Mohamed Nassor, Mulamu Ng'ambi, Octavian Mshiu, Profesa Mohamed Janabi, Hassan Kipusi, Gerald Yambi, Moses Kaluwa, Crescentius Magori, na Idd Kajuna.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (katikati), akizindua Kampeni ya NMB MastaBata – Halipoi, yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya kadi badala ya fedha taslimu, uzinduzi huo ulifanyika kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Madaraka Tanga, Elizabeth Chawinga, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Baraka Ladislaus na Kaimu Katibu Tawala Wilaya ya Tanga, Leornad Sembe. Kutoka kulia ni Mkuu wa Idara ya Bima NMB, Martine Massawe, Meneja Uhusiano na Serikali wa Kanda ya Kaskazini, Christabel Hiza na Mkuu wa Idara ya Kadi wa NMB, Philbert Casmir. **MPIGAPICHA WETU**

## Wateja NMB kujishindia milioni 350/- MastaBata

**Na Mwandishi Wetu,** Tanga

BENKI ya NMB imezindua rasmi msimu wa tano wa promosheni yake kabambe ya 'MastaBata' chini ya kauli mbiu 'MastaBata Halipoi' inayolenga kuwazawadia wateja wake kwa uaminifu wanaoonyesha.

Katika promosheni hiyo ya miezi mitatu ambayo itafikia kilele Januari 25, mwaka huu, wateja wa benki hiyo watajishindia zaidi ya fedha taslimu shilingi milioni 350 pamoja na safari zilizolipiwa kila kitu za kula bata katika 'full moon party' huko Kendwa Rocks visiwani Zanzibar na safari za kwenda hadi Jiji la Cape Town, Afrika Kusini wakati wa droo ya mwisho.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Tanga mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Idara ya Biashara ya Kadi wa Benki ya NMB, Philbert Casmir, alisema kampeni hiyo si tu inaendana na malengo ya Tanzania ya kuwa na uchumi usio wa matumizi ya fedha taslimu bali ni hatua muhimu katika kuongeza kasi ya ushirikishwaji wa kifedha.

"Hi promosheni yetu inalenga kuchochea matumizi ya malipo ya kidijitali ambayo yameonekana kuwa rahisi zaidi, ya haraka na salama pamoja na aina mbalimbali za malipo ya kidigitali zinazopatikana kwa urahisi kwetu.

"Ninawahimize sana wateja wetu kutumia NMB MasterCard kulipia bidhaa au huduma kupitia mashine za mauzo (POS), Msimbo wa QR au mamunuzi ya mtandao ili kujiwekea nafasi nzuri ya kujishindia pesa taslimu na safari zilizolipiwa kila kitu wakati wa kampeni," alisema Casmir.

Casmir alibainisha kuwa promosheni hiyo ni njia ya kuwazawadia wateja waaminifu wa benki hiyo kwa kuendelea kuwaunga mkono kwa muda mrefu na kuongeza kuwa benki ya NMB imeweza kupiga hatua kubwa katika miaka yake 25 ya utendaji kazi wake kutokana ina imani ya wateja.

## Robertinho aitaja Yanga 'sab'

INATOKA UKURASA 24

kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ambayo yatawasaidia kufikia malengo yao mwisho wa msimu.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema japo wachezaji walikuwa na uchovu, walicheza kwa mipango na kutafuta ushindi huku benchi la ufundi wakiitumia kama sehemu ya maandalizi ya mechi ijayo dhidi ya Yanga.

"'Chalenji' ipo, ligi ni ngumu kila timu imejipanga, inakuja kivingine na kubadilika ni jambo jema kwa sababu inaonesha ubora wa ligi yetu, hatukutarajia kuona Namungo FC anashinda dhidi ya Azam FC.

"Sisi Simba tunaenda kwa mipango, hatutaki kukurupuka kila mechi unaingia na mbinu zake tukishinda moja sawa kikubwa ni alama tatu. Hii mechi ya leo (juzi), imekuwa sehemu ya kujiandaa na 'dabi' dhidi ya watani wetu," alisema Try Again.

Aliongeza kuwa Dabi ya Kariakoo ni mechi kubwa na wanaiheshimu, hivyo wataitendea haki ili kutoa ramani ya ubingwa, kwa kuwa wako makini kwa mechi kubwa na ngumu na ambaye atacheza vizuri atapata matokeo mazuri.



"Wapinzani wetu wako vizuri, wachezaji wanapambana na wanajituma kutafuta ushindi, Simba tumejipanga vizuri na itakuwa mechi ya burudani kwa mashabiki wetu, wasije kusahau ni mechi yetu tuko nyumbani.

"Niwaombe Wanasimba wajitokeze kwa wingi robo tatu ya uwanja iwe nyeupe na nyekundu ili wachezaji wetu wapate nguvu na kuona sapoti kubwa kuliko mechi za awali," alisema Mwenyekiti huyo.


# Michezo

Jumatatu Oktoba 30, 2023

Nipashe



'Nilijua Nketiah ataibeba Arsenal' UKURASA 21



BALEKE

AZIZ KI

# Baleke, Aziz Ki raha dabi Simba, Yanga

**Adam Fungamwango**

## ●●● Kushuka dimbani kitakwimu wakiwa sawa, mizani ya timu hizo nayo 'yabalansi', lakini...

WAKATI habari ya mjini kwa upande wa soka kwa sasa ikiwa ni mechi ya 'dabi' ya Simba na Yanga Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, takwimu za timu hizo pamoja na wachezaji wao wawili; mshambuliaji Jean Baleke na kiungo mshambuliaji, Stephane Aziz Ki, zinafurahisha na kuleta msisimko mkubwa kuelekea mchezo huo.

**Ipo hivi, Jumapili Simba na Yanga zitacheza mechi hiyo ya mzunguko wa kwanza zikiwa na vitu vingi inavyofanana mpaka sasa.**

Timu zote zina pointi 18, lakini Yanga ikikaa juu kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kutokana na kuwa na mabao mengi ya kufunga, ikipachika mabao 20 na kuruhusu manne, huku wapinzani wao wakicheka na nyavu mara 16 na kuruhusu matano.

Hata hivyo, Yanga yenyewe pointi zake 18 imezipata kutokana na michezo saba iliyocheza hadi sasa, huku Simba yenyewe ikivuna alama hizo kutokana na kushuka dimbani mara sita tu.

Aidha, timu hizo zina wachezaji walio juu ya orodha ya wafungaji bora wa mabao msimu huu, Baleke kwa upande wa Simba na Aziz Ki upande wa Yanga kila mmoja akiwa amefumania nyavu mara sita, hivyo kama wakipata nafasi ya kucheza itakuwa ni vita nyingine ya kuamua nani atamwacha mwezake na kutawala kileleni.

Ni wachezaji hao hao ambao wana 'hat-trick' kila mmoja, Baleke akiipata katika mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, Agosti 17, mwaka huu Simba ikishinda mabao 4-2, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro na Aziz Ki, akiipata Jumatatu iliyopita Uwanja wa Benjamin Mkapa akiiongoza timu yake kushinda mabao 3-2 dhidi ya Azam FC.

Mara ya mwisho Simba na Yanga zilikutana kwenye mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii, Agosti 13, mwaka huu katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Simba ikishinda mabao 3-1 kwa mikwaju ya penalti, baada ya kutoa suluhu ndani ya dakika 90 za mchezo.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Muargentina Miguel Gamondi juzi

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho aitaja Yanga 'sab' ya Kibu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuvuna pointi tatu dhidi ya Ihefu FC, kocha na uongozi wa Simba umeweka wazi kuwa mechi hiyo ilikuwa sehemu ya maandalizi kwa mchezo ujao wa dabi na ushindi walioupata ni salamu kuelekea mchezo wa watani wa jadi Jumapili wiki hii dhidi ya Yanga.

Umesema licha ya ubora wa Yanga, hawana kitu kingine zaidi ya kuhitaji ushindi kwani ndicho pekee kitakachowapeleka kwenye ramani za mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba iliendelea kupata ushindi katika mchezo wake wa sita mfululizo juzi kwa kuifunga Ihefu FC mabao 2-1, kwenye mechi iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ukiwa ni ushindi wa asilimia 100 msimu huu.

Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, alifurahia ushindi huo dhidi ya Ihefu kutokana na mchezo kuwa mgumu huku akisema sasa anaenda kuandaa silaha zake kwa ajili ya dabi dhidi ya Yanga.

Robertinho alisema wanapata muda mfupi wa kujiandaa kabla ya mechi kutokana na ratiba kubana, lakini kikubwa ni pointi tatu zimepatikana.

Alisema mchezo wa juzi ilibidi kuwapumzisha baadhi ya nyota akiwamo Kibu Denis na Jean Baleke katika dakika 45 ili kuwaandaa kwa ajili ya mchezo unaofuata wa dabi.

"Ratiba ni ngumu, tumetoka kushiriki michuano mikubwa ya African Football League (AFL), na tumefanya mazoezi siku mbili kabla ya leo kushuka uwanjani.

"Ndio maana nawapongeza wachezaji wangu, haikuwa kazi rahisi, lakini kikubwa tumepata pointi tatu muhimu nyumbani," alisema Robertinho.

Robertinho alisema baada ya kukamilika kwa dakika 90 dhidi ya Ihefu FC, sasa wanajiandaa na mchezo ujao dhidi ya Yanga,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >